Historia ya Tanzania na Maadili

Kitabu cha Mwanafunzi

Darasa la 3





Taasisi ya Elimu Tanzania

02/12/2023 16:52

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Historia ya Tanzania na Maadili

Kitabu cha Mwanafunzi

Darasa la 3

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

Cheti cha Ithibati

Na. 1177

Jina la Chapisho: Historia ya Tanzania na Maadili Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tatu

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978-9987-09-950-4

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 23 Oktoba, 2023 kuwa Kitabu cha Kiada kwa ajili ya Mwanafunzi wa Darasa la Tatu katika ngazi ya Elimu ya Msingi nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa Mwaka 2023.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2023

Toleo la Kwanza 2023

ISBN: 978-9987-09-950-4

Taasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S. L. P. 35094
14112 Dar es Saalam

Simu: +255- 735041168/+255- 735041170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha wala kutafsiri kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Taasisi ya Elimu Tanzania.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 2 27/11/2023 12:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Yaliyomo

Shukurani iv

Utangulizi v

Sura ya Kwanza **1**
Dhana ya Historia ya Tanzania na Maadili 1

Sura ya Pili **24**
Urithi wa Tanzania 24

Sura ya Tatu **45**
Wajibu na haki za mtoto 45

Sura ya Nne **59**
Matendo ya kuthamini maadili 59

Sura ya Tano **71**
Maarifa na ujuzi wa asili wa jamii 71

Sura ya Sita **92**
Asili za jamii za Watanzania 92

Sura ya Saba **108**
Urithi na asili za jamii kwa maendeleo ya sasa 108

Sura ya Nane **118**
Uhusiano na ushirikiano na jamii 118

Sura ya Tisa **133**
Kukuza na kutunza maadili ya jamii 113

FOR ONLINE USE ONLY

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 3 27/11/2023 12:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki kutoka taasisi mbalimbali za umma na binafsi walioshiriki kufanikisha uandishi wa Kitabu cha Mwanafunzi cha Historia ya Tanzania na Maadili, Darasa la Tatu. Kipekee TET inatoa shukurani kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu Mzumbe (Morogoro), Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule, vyuo vya ualimu na shule za msingi. Pia, TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wafuatao:

Waandishi: Dkt. Joyce J. Kahembe, Bw. Castor A. Lyuma, Bi. Edna M. Mathew na Bw. Boniventure A. Bazira

Wahariri: Dkt. Evaristi Magoti na Dkt. Musa Sadock

Msanifu: Bw. Amani Kweka

Wachoraji: Bw. Fikiri A. Msimbe, Bw. Yohana P. Mwenda na Bw. Gwakisa U. Mwandoloma

Mratibu: Dkt. Joyce J. Kahembe

Vilevile, TET inatoa shukurani kwa walimu wote wa shule za msingi na wanafunzi walioshiriki katika ujaribishaji wa kitabu hiki. Mwisho, TET inaishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha zilizofanikisha kazi ya uandishi na uchapaji wa kitabu hiki.

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
Taasisi ya Elimu Tanzania

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 4 27/11/2023 12:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Utangulizi

Kitabu hiki cha Historia ya Tanzania na Maadili kimeandikwa mahususi kwa ajili ya mwanafunzi wa Darasa la Tatu, Tanzania Bara. Kitabu hiki kimeandaliwa kulingana na muhtasari wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili uliotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia mwaka 2023.

Kitabu hiki kina sura tisa, ambazo ni dhana ya Historia ya Tanzania na Maadili, urithi wa Tanzania, wajibu na haki za mtoto, matendo ya kuthamini maadili, maarifa na ujuzi wa asili wa jamii, asili za jamii za Watanzania, urithi na asili za jamii kwa maendeleo ya sasa, uhusiano na ushirikiano na jamii, na kukuza na kutunza maadili ya jamii. Kwa kujifunza maudhui ya kitabu hiki utamudu maarifa, stadi na mwelekeo wa kuwa mzalendo, kujenga maadili, kukuza utaifa na kulinda maslahi ya nchi na rasilimali za Taifa. Hivyo, kuweza kuishi katika misingi ya utu, uadilifu, umoja, upendo na kuthamini rasilimali za Taifa.

Maudhui ya sura hizi yamewasilishwa kwa njia ya matini, kazi za vitendo, picha zenye mvuto, pamoja na mazoezi. Hivyo, unapaswa kufanya mazoezi na kazi zote zilizopo kwenye kitabu hiki pamoja na kazi nyingine utakazopewa na mwalimu. Hii itakuwezesha kukuza maarifa na stadi zinazokusudiwa.

FOR ONLINE USE ONLY

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 5 27/11/2023 12:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Jifunze zaidi kupitia maktaba mtandao
http://ol.tie.go.tz au ol.tie.go.tz

Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE USE ONLY

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 6 27/11/2023 12:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Sura ya Kwanza

Dhana ya Historia ya Tanzania na Maadili

Utangulizi

Katika sura hii utajifunza kuhusu dhana ya Historia ya Tanzania na Maadili. Pia, utajifunza kuhusu vitendo vya kimaadili. Vilevile, utajifunza umuhimu wa Historia ya Tanzania na Maadili nchini. Umahiri utakaoupata katika sura hii utakuwezesha kuthamini Historia ya Tanzania, Maadili ya Tanzania na kutenda vitendo vya maadili.



Fikiri

Dhana ya Historia ya Tanzania na Maadili.

Kazi ya kufanya namba 1



Fanya uchunguzi mdogo kuhusu tukio mojawapo unalolikumbuka katika maisha yako, kisha wasilisha darasani.

Matukio tuliyoyaandika yanaonesha mfululizo wa mambo yaliyotokea katika maisha yetu katika vipindi tofauti. Mfululizo huu wa matukio ni sehemu ya historia ya maisha yetu. Ni historia kwa sababu matukio haya yanajenga kumbukumbu katika maisha yetu. Historia inaweza kuhusu maisha yetu binafsi, familia, shule, jamii inayokuzunguka, nchi au dunia.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 1 27/11/2023 12:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kazi ya kufanya namba 2



Andika matukio yaliyotokea na kuacha kumbukumbu katika shule yako.

Matukio tuliyoorodhesha ni sehemu ya historia katika shule yetu. Matukio haya ni sehemu ya historia ya shule yetu kwa kuwa yameacha alama ya kumbukumbu katika shule.

Dhana ya Historia ya Tanzania na Maadili imeundwa na dhana ya historia ya Tanzania na dhana ya maadili. Dhana ya historia ya Tanzania imebeba maana, matukio ya kihistoria Tanzania na umuhimu wa historia ya Tanzania. Dhana ya pili inahusu maadili, ambayo imebeba maana, vitendo vya maadili na umuhimu wa maadili nchini. Tunapojifunza dhana hizi kwa pamoja, tunapata nafasi ya kubaini maadili yetu na misingi ya ujenzi wa maadili katika historia ya jamii za Kitanzania. Hivyo, kuiwezesha jamii ya sasa kukuza na kulinda maadili ya Watanzania kwa sasa.

Maana ya historia ya Tanzania

Inawezekana umewahi kusikia kuhusu Historia ya Tanzania au maeneo yenye historia ya Tanzania. Historia ya Tanzania ni nini?

Kazi ya kufanya namba 3



Soma matini kutoka katika vyanzo mbalimbali, ikiwemo mtandao, kuhusu maana ya historia ya Tanzania.

Historia ya Tanzania ni elimu kuhusu matukio yaliyotokea nchini Tanzania tangu mwanzo wa maisha ya watu mpaka

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 2 27/11/2023 12:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

leo. Pia, inahusu namna matukio hayo yalivyotokea. Kwa ujumla, historia ya Tanzania ina mfululizo wa matukio yaliyotokea katika nchi na jinsi yalivyotokea. Mfululizo huo ndio uliounda uthibitisho wa historia ya Taifa la Tanzania tulilonalo kwa sasa. Mfululizo na muunganiko wa matukio haya ndio historia ya Tanzania. Tutajifunza kuhusu matukio ya kiuchumi, kijamii na kisiasa yenye kumbukumbu za historia ya Tanzania. Je, unafikiri kuna umuhimu gani wa kujifunza historia ya Tanzania?

Umuhimu wa kujifunza Historia ya Tanzania

Kazi ya kufanya namba 4



Fanya uchunguzi kutoka katika vyanzo mbalimbali kwa kusoma matini na maktaba mtandao na eleza umuhimu wa kujifunza historia ya Tanzania.

Mara nyingi tunashindwa kuanza jambo jipya kwa kukosa taarifa za awali. Mambo tunayoyaona sasa yanaweza kuwa yamewahi kutokea zamani. Taarifa za kihistoria ni muhimu kwetu, kwa jamii na Taifa. Hivyo, kujifunza historia ya Tanzania ni muhimu kwa sababu inatupa:

(a) Taarifa za matukio yaliyotokea zamani na jinsi yalivyotokea;

(b) Funzo la kutuwezesha kuendeleza mambo mazuri;

(c) Elimu ya kuboresha mipango ya sasa na kupata matokeo mazuri;

(d) Elimu ya kukabili changamoto tunazokutana nazo kwa sasa;

(e) Dira ya kutatua mambo ya sasa;

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 3 27/11/2023 12:18

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(f) Sababu ya kufanya maamuzi sahihi kwa sasa;

(g) Kukuza na kulinda uzalendo kwa sasa;

(h) Kuthamini historia kama sehemu ya urithi wa Taifa; na

(i) Kukuza na kulinda mila na desturi kama sehemu ya maadili yetu.

Vyanzo vya Historia ya Tanzania

Tunaweza kupata taarifa za historia ya Tanzania kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo kusikiliza masimulizi au kusoma vitabu. Pia, katika makumbusho ya Taifa na binafsi na maeneo yenye hifadhi za nyaraka kuna taarifa za kihistoria. Tunaweza kupata taarifa za historia kutoka kwenye taarifa za kianthropolojia, akiolojia na isimu historia. Vilevile, tunaweza kuuliza watu waliotangulia ili kupata taarifa hizi. Vyombo vya habari na tovuti vinaweza pia kuwa ni vyanzo vya kupata taarifa hizo. Vyanzo hivi vinawezesha kujifunza historia ya Tanzania ya nyakati tofauti kama vile kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni.

Dhana ya maadili

Kazi ya kufanya namba 5



Soma vyanzo mbalimbali, ikiwemo maktaba mtandao, kuhusu maana ya maadili.

Maadili ni mwenendo au utendaji uliokubalika katika jamii. Maadili hueleza matendo yanayofaa na matendo yasiyofaa katika jamii husika. Maadili yanaweza kulenga katika tabia au matendo ya kufuata katika familia, shule, dini, jamii au Taifa. Maadili huwezesha watu kuishi kwa kuzingatia utu, upendo na tabia njema. Ujenzi wa maadili si jambo la muda

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 4 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mfupi, bali hufanyika kwa kipindi fulani na kukubaliwa na jamii nzima kuwa ndizo tabia, kanuni na sheria za kikundi au jamii husika.

Soma matendo yanayofaa na yasiyofaa katika sehemu A, kisha fanya zoezi linalofuata.

A	B	C
Matendo yanayofaa na yasiyofaa	Matendo yanayofaa	Matendo yasiyofaa
kufanya kazi, kutoroka nyumbani, kucheza, kuwaheshimu watu waliokuzidi umri, kuchelewa kurudi nyumbani, kufanya kazi za nyumbani, kuwasalimia watu wengine, kuwatukana watu wengine, kuwafinya wenzako, kusema ukweli, kupigana na wenzako, kuiba, kutokupenda kufanya kazi, kuwahi shuleni, kuwatembelea wagonjwa, kuacha kuwasalimia wenzako, kuacha kuwasalimia watu waliokuzidi umri, kuacha vyombo mezani baada ya kula, kukataa kula chakula, kuosha chombo chako baada ya kula, kuacha kufanya usafi, kuwanyanyasa na kuwadhalilisha wenzako, kuwasaidia wasiojiweza, kutoroka shuleni, kusema uongo, kutokumaliza mazoezi ya darasani		

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 5 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Zoezi la 1

1. Andika matendo yanayofaa katika sehemu B na yasiyofaa katika sehemu C.
2. Eleza ni kwa nini matendo yaliyoorodheshwa katika sehemu B ni matendo yanayofaa.
3. Eleza ni kwa nini matendo yaliyoorodheshwa katika sehemu C ni matendo yasiyofaa.

Matendo yanayozingatia kanuni, taratibu na sheria zilizowekwa katika familia, shule au jamii ni matendo yanayofaa. Matendo hayo ni nguzo ya kujenga maadili na kuondoa ugomvi katika mazingira yanayotuzunguka. Maadili ya jamii zetu husisitiza uzingatiaji wa kanuni, miongozo, mila na desturi za jamii husika. Tabia zisizozingatia maadili ya familia, shule au jamii ni matendo yasiyofaa. Maadili katika jamii husisitiza matendo yanayofaa. Lengo ni kuiwezesha jamii kuishi katika misingi ya utu, uadilifu, umoja, upendo, usawa na amani.

Vitendo vya kimaadili

Kazi ya kufanya namba 6



Chunguza na andika vitendo vya kimaadili vinavyofanywa shuleni au nyumbani.

Vitendo vya kimaadili vinahusisha tabia na vitendo ambavyo vinakubalika katika jamii. Vitendo vya kimaadili hutofautiana kulingana na tamaduni za kila jamii.

Kusaidia wazee na watu waliotuzidi umri

Kusaidia wazee na watu waliotuzidi umri ni mojawapo ya matendo ya kimaadili. Vijana au watoto wanawajibika kuwasaidia mizigo na kazi mbalimbali watu waliowazidi umri,

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 6 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

nyumbani na shuleni. Kitendo cha kijana au mtoto kumsaidia mzee na mtu aliyemzidi umri huonesha upendo na heshima kama ilivyo katika Kielelezo namba 1.



Kielelezo namba 1: *Mtoto akimsaidia mzigo mzee*

Kuwatunza, kuwathamini na kuwalea wazee ni matendo ya kimaadili. Maadili yanasisitiza kutembelea wazee na kuwahudumia kwa kuwapa zawadi na chakula kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 2. Pia, tunasisitizwa kuwasaidia kazi mbalimbali.



Kielelezo namba 2: *Kijana akimwandalia mzee chakula*

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 7 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kuheshimu watu wazima

Kuwaheshimu wazee na watu waliokuzidi umri ni matendo ya kimaadili. Watu walio na umri mdogo wanawajibika kuwaheshimu watu waliowazidi umri. Tangu kale, watu wenye umri mkubwa waliheshimika. Jamii iliamini kuwa watu wenye umri mkubwa wana maarifa, busara na ufahamu wa mambo zaidi ya wenye umri mdogo. Mfano, vijana walilazimika kuwapisha viti watu waliowazidi umri ili kuonesha heshima. Ilikuwa ni jambo la aibu kwa kijana kukaa kwenye kiti wakati watu waliomzidi umri wamesimama kama ilivyo katika Kielelezo namba 3 (a).



Kielelezo namba 3 (a): *Vijana wamekaa wakati mtu mzima amesimama*

Vijana walitakiwa kuwapisha viti watu wenye umri mkubwa kama ilivyo katika Kielelezo namba 3 (b). Hii ilionesha heshima na adabu kwa watu wazima.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 8 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Kielelezo namba 3 (b): *Kijana amesimama kumpisha mtu mzima kiti akae*

Pia, wazazi waliitwa kwa majina ya watoto wao, kama vile mama Juma au baba Bahati. Hii ilifanyika ili kuwapa heshima kama wazazi. Vilevile, ilikuwa mwiko na jambo lisiloonesha heshima wazazi kuitwa kwa majina yao na watoto au vijana.

Kusalimiana

Kusalimiana ni mojawapo ya matendo ya maadili. Wadogo kwa umri walitakiwa kusalimia waliowazidi umri. Pia, watu wa rika moja walisalimiana ili kuonesha kujali na utu kwa watu wengine. Jamii zilisalimiana nyakati zote, asubuhi, mchana na jioni. Wanajamii walisalimiana kwa ama kushikana mikono, kupiga goti, kushika kichwa, kusimama, kukaa chini au kukumbatiana ili kuonesha heshima. Angalia mfano wa matendo ya kusalimiana katika Kielelezo namba 4.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 9 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE





Kielelezo namba 4: *Vitendo vya maadili katika kusalimiana*

Tofauti katika matendo ya kusalimiana hutegemea tamaduni za jamii husika. Mtoto alipaswa ama kusimama au kupiga goti anaposalimia watu waliomzidi umri. Kitendo cha kijana kukaa wakati anamsalimia mtu mzima si kitendo cha kimaadili ya Kitanzania.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 10 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Zoezi la 2

1. Taja vitendo vya kimaadili vinavyoonesha heshima vinavyofanyika shuleni.
2. Taja vitendo vya kimaadili vinavyoonesha heshima vinavyofanyika nyumbani.

Vitendo vya maadili katika malezi na ulinzi wa watoto

Malezi na ulinzi wa watoto ni sehemu ya matendo ya kimaadili. Tangu kale jamii zilisisitiza malezi ya watoto. Wazazi walitenga muda wa kukaa na watoto wao. Hii iliwasaidia wazazi na watoto kukaa na kuongea pamoja mambo yanayohusu familia na kujua changamoto zao kama ilivyo katika Kielelezo namba 5.



Kielelezo namba 5: *Wazazi na watoto wakiongea pamoja*

Pia, wazazi wanawajibika kulinda usalama wa watoto wakati wote. Ulinzi na malezi ya watoto katika jamii ulifanyika kwa

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 11 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kushirikiana na lilikuwa jukumu la jamii nzima. Hata sasa jamii inapaswa kulinda usalama wa watoto. Mfano, wazazi wana wajibu wa kuwapeleka watoto shuleni kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 6 na kuwafuata wakati wa kurudi nyumbani ili kuwalinda. Pia, ni muhimu kuweka mifumo imara katika jamii ili kulinda usalama wa watoto shuleni na nyumbani.



Kielelezo namba 6. *Watoto wakipelekwa shuleni na mzazi*

Vitendo vya maadili katika kazi

Kufanya kazi kwa bidii ni jambo lililosisitizwa katika maadili ya jamii. Tabia ya kupenda na kufanya kazi ni matendo ya kimaadili katika jamii. Hivyo, kila mtu anapaswa kupenda na kufanya kazi kwani kazi ni msingi wa maendeleo. Tangu kale, uvivu ulipingwa na jamii nzima. Watu katika jamii walithaminiwa kutokana na uwezo wao wa kufanya kazi. Mtu mvivu alipingwa kwa kukiuka maadili ya jamii. Viongozi walichaguliwa kwa kuzingatia uwezo wao wa kufanya kazi. Kielelezo namba 7 kinaonesha watoto wakifanya kazi mbalimbali nyumbani.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 12 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Kielelezo namba 7: *Watoto wakifanya kazi mbalimbali nyumbani*

Matendo ya maadili katika kusaidiana

Jamii zetu zinasisitiza matendo ya kuwasaidia watu wengine na kusaidiana. Kuwasaidia watu wenye mahitaji maalumu ni sehemu ya maadili ya jamii za Kitanzania. Kila mmoja anao wajibu wa kuwasaidia watu wanaohitaji msaada kama ilivyo katika Kielelezo namba 8. Kuwasaidia watu wengine kunasaidia watu kupendana, kusaidiana na kushikamana.



Kielelezo namba 8: *Wanafunzi wakimsaidia mwanafunzi mwenzao*

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 13 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kazi ya kufanya namba 7

Andika matendo mengine ya kimaadili katika kusaidiana shuleni na nyumbani.

Kuhusiana na watu wengine

Uhusiano mwema ni sehemu ya matendo ya kimaadili. Uhusiano mwema huzuia malumbano na ugomvi kati ya mtu na mtu. Uhusiano mwema kati yetu hujengwa kwa kuonesha upendo, kuheshimiana na kutosema uongo dhidi ya watu wengine. Pia, matendo kama kuwasiliana kwa lugha isiyo ya ukali na matusi na kuwasikiliza watu wengine yanaashiria uhusiano mwema. Vilevile, matendo ya kucheza na kusoma pamoja huonesha uhusiano mwema kati yetu na watu walio karibu nasi.

Chunguza matendo katika picha zifuatazo katika Kielelezo namba ९, kisha jibu zoezi linalofuata.



Kielelezo namba ९: *Matendo ya kuhusiana shuleni*

Zoezi la 3

1. Eleza matendo yanayofanyika katika Kielelezo namba ९.
2. Eleza faida za matendo yanayofanyika katika Kielelezo namba ९.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 14 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kushirikiana

Kazi ya kufanya namba 8

Fanya uchunguzi katika maeneo yanayokuzunguka na eleza matendo ya maadili katika kushirikiana.

Ushirikiano katika kazi mbalimbali kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 10 ni miongoni mwa vitendo vya kimaadili.



Kielelezo namba 10: *Wanafunzi wakishirikiana kazi shuleni*

Ni wajibu wetu kushirikiana katika kazi za shuleni na nyumbani. Jamii za kale zilishirikiana katika kazi zilizofanyika katika maeneo yao, kama vile kufanya usafi, kuchimba visima na kutengeneza barabara. Watu wote katika jamii wanaume, wanawake na watoto, walitakiwa kufanya kazi hizi kwa pamoja.

Pia, ushirikiano ulifanyika katika shughuli za sherehe, misiba na mazishi kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 11.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 15 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Kielelezo namba 11: Watu wakishirikiana katika msiba

Hapo kale, mtu ambaye hakushiriki katika misiba alipewa adhabu. Pengine alitengwa na jamii yote na hata kutozwa faini. Kushiriki katika misiba ni mojawapo ya vitendo vya kimaadili kwa sababu huonesha hali ya kujali na kufariji watu wengine. Tunaposhiriki misiba, tunatakiwa kusaidia kazi kwa hali na mali. Ushiriki unaweza kuwa katika kuchimba kaburi, kupika chakula na kuchota maji. Pia, tunasisitizwa kwenda kwenye misiba na chakula, maji, mafuta, kuni, fedha na mahitaji mengine. Hii inasaidia kuwezesha kufanyika kwa shughuli za msiba kwa wafiwa. Hapo kale ilikuwa ni mwiko na aibu kwenda msibani mikono mitupu.

Vilevile, kushirikiana katika sherehe ni vitendo vya kimaadili. Tangu kale, jamii zilisisitiza kushirikiana katika sherehe kama vile harusi na sherehe za mavuno. Watu walishirikiana katika sherehe kwa kutoa mchango, zawadi na vitu mbalimbali ili kufanikisha sherehe. Ushirikiano ni jambo muhimu katika jamii. Jamii kwa sasa inaweza kukuza ushirikiano kwa kushiriki

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 16 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

katika shughuli mbalimbali za kijamii. Ushirikiano hujenga upendo na umoja katika jamii.

Kazi ya kufanya namba 9



Jadili namna runinga, radio, muziki wa kizazi kipya, tamthilia, simu janja, katuni na matangazo mbalimbali yanavyochangia katika kuharibu na kukuza maadili nchini Tanzania kwa sasa.

Vyombo vya habari na matangazo vina athari mbalimbali katika maadili ya jamii kwa sasa. Watoto wana wajibu wa kuacha kuiga tabia zisizofaa ili kujenga tabia njema katika jamii ya sasa. Matendo yasiyofaa yana athari kubwa kwa mtoto, familia na jamii kwa ujumla. Pia, sisi sote tuna wajibu wa kuwaeleza watoto wengine kuacha vitendo vilivyo kinyume na maadili ili kujenga maadili yanayofaa nchini.

Kukataa vitendo vya rushwa

Rushwa ni kitendo cha kutoa au kupokea fedha au kitu cha thamani ili kutenda kitendo kilicho kinyume na haki ya mtu mwingine. Pia, kuombwa fedha au kitu cha thamani na mtu mwingine ili kupata haki usiyostahili ni vitendo vya rushwa. Kukataa vitendo vya kutoa na kupokea rushwa ni matendo ya kimaadili. Vitendo vya kutoa na kupokea rushwa hufanyika kwa lengo la kufanya upendeleo kwa anayetoa rushwa na kwa lengo la kumnyima mtu mwingine haki yake. Vitendo hivyo vinaweza kufanyika shuleni, nyumbani na maeneo mengine yanayotuzunguka.

Kazi ya kufanya namba 10



Chunguza na orodhesha vitendo vinayoashiria rushwa nyumbani na shuleni.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 17 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Vitendo vinavyoashiria rushwa ni pamoja na:

(a) Kumpatia au kupokea kitu kutoka kwa mtu mwingine mfano pipi au biskuti, ili kufanya vitendo visivyostahili au vilivyo kinyume na maadili;

(b) Kupewa au kupokea kitu ili uandikiwe au umwandikie mwanafunzi mwenzako majibu ya kazi za darasani;

(c) Kudai zawadi au fedha ili kutekeleza jambo fulani; mfano, kukubali kutumwa;

(d) Kununuliwa kitu kama vile chakula au zawadi na mtu mwingine kwa ushawishi wa kufanya vitendo visivyofaa;

(e) Kupewa lifti katika vyombo vya usafiri mara kwa mara na mtu mwingine ili kufanya vitendo visivyo vya kimaadili;

(f) Walimu kuwapa wanafunzi majibu ya mtihani kwa malipo fulani;

(g) Kutoa fedha au zawadi ili kupata upendeleo wa ziada kutoka kwa walimu, viranja, wazazi au walezi;

(h) Kupokea fedha au zawadi ili kuwafanyia watu wengine vitendo vilivyo kinyume na maadili;

(i) Mwalimu au mwanafunzi ambaye ni kiranja kupokea fedha au zawadi ili kuruhusu mali za shule kama vile vitabu, redio au televisheni kuchukuliwa na kupelekwa nyumbani kwa matumizi binafsi;

(j) Mlinzi wa shule kupokea fedha au kuahidiwa kupewa fedha ili kuruhusu vifaa vya shule kama taa, madawati, au mbao na saruji za kujengea miradi ya shule kuchukuliwa shuleni;

(k) Kupewa zawadi ili kuacha kutoa taarifa za uhalifu kwa uongozi wa shule au kwa wazazi nyumbani;

(l) Mwanafunzi kutoa au kumpa zawadi mwalimu au kiranja ili asipewe adhabu kwa kosa alilolifanya; mfano, kuchelewa kufika shuleni au kupiga kelele darasani;

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 18 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(m) Mwanafunzi au mzazi kutoa au kumpa zawadi mwalimu ili atoe alama za upendeleo kwa mwanafunzi; na
(n) Dada mlezi nyumbani kupokea fedha au mali kama simu kutoka kwa mtoto na kumruhusu aende kucheza wakati mzazi ameelekeza mtoto huyo abaki nyumbani na kukamilisha kwanza kazi za shuleni na za nyumbani kabla ya kwenda kucheza.

Vitendo vya kutoa na kupokea rushwa vina madhara kwetu na kwa jamii inayotuzunguka. Baadhi ya madhara yanayoweza kutokea unapotoa au kupokea rushwa ni pamoja na:

(a) Kushindwa kupata wanafunzi waliofaulu mitihani kwa akili zao;
(b) Miradi ya shule kama vile madarasa kushindwa kukamilika kwa wakati;
(c) Kukosa wataalamu wenye uwezo stahiki nchini kutokana na wanafunzi kupata alama za mitihani wasizostahili;
(d) Kusababisha watu wengine kukosa haki zao kwa sababu ya kukosekana kwa usawa katika jamii;
(e) Kuwepo kwa mmomonyoko wa maadili katika jamii kwa sababu ya kulea uzembe shuleni na nyumbani; na
(f) Kukosekana kwa maendeleo katika familia au jamii kutokana na kukosa watu sahihi wa kuleta maendeleo.

Zoezi la 4

1. Taja madhara mengine matatu ya vitendo vya rushwa.

Mwanafunzi ana wajibu wa kuzuia vitendo vya rushwa katika maeneo yanayomzunguka shuleni na nyumbani. Tunaweza kufanya mambo yafuatayo ili kuepuka na kuzuia vitendo vya rushwa:

(a) Kufuata na kuheshimu sheria, kanuni na taratibu za shule na familia;

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 19 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Kusoma kwa bidii ili kuweza kufaulu mitihani bila kutafuta upendeleo;
(c) Kutotoa zawadi au pesa ili kupata upendeleo wa aina yoyote;
(d) Kumjulisha mwalimu, mzazi au mtu mwingine unayemwamini kuhusu jambo baya alilofanya mwanafunzi, mwalimu, mfanyakazi wa shule au ndugu nyumbani;
(e) Kusema ukweli wakati wote bila upendeleo ili kuwa sehemu ya msaada wa watu kupata haki zao inavyostahili;
(f) Kuwatendea mema watu wengine bila kuwa na upendeleo;
(g) Kuwaheshimu na kuwapenda watu wengine;
(h) Kukemea vitendo vya rushwa;
(i) Kupenda shule na familia kwa kuthamini na kutunza mali za nyumbani na za shuleni; na
(j) Kufanya kazi kwa bidii ili kupata mahitaji yako bila upendeleo.

Kuepuka rushwa ni vitendo vya kimaadili. Mtu anayeshiriki vitendo vya rushwa hana maadili. Mtu mwenye maadili huepuka vitendo vya rushwa ambavyo vinaweza kuleta madhara kwake, kwa watu wengine, jamii na Taifa kwa ujumla.

Umuhimu wa vitendo vya kimaadili

Vitendo vya kimaadili vinajenga tabia za malezi bora kwa watoto. Malezi hayo ni pamoja na kuwafundisha watoto matendo yanayofaa. Tunapaswa kuendeleza vitendo vya kimaadili shuleni na nyumbani.

Kazi ya kufanya namba 11



Chunguza na eleza umuhimu wa vitendo vya kimaadili vinavyofanyika shuleni na nyumbani.

Vitendo vya kimaadili ni muhimu katika maisha yetu. Vitendo hivi hujenga umoja katika jamii bila ya kujali tofauti za kijinsi,

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 20 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kiimani, kielimu au rangi. Vitendo vya kimaadili ni muhimu kwa sababu husaidia:

(a) Jamii kufanya na kuthamini kazi;
(b) Kuleta usawa katika jamii bila kujali hali ya mtu;
(c) Kujenga tabia ya kuheshimiana na kuhusiana;
(d) Kujenga malezi bora katika jamii;
(e) Kulinda na kuimarisha maadili katika jamii;
(f) Kujenga tabia ya mshikamano na moyo wa kusaidiana katika jamii; na
(g) Kujenga undugu na upendo katika jamii.

Kazi ya kufanya namba 12



Andika mambo uliyojifunza kuhusu vitendo vya maadili na jinsi ya kudumisha maadili hayo nyumbani na shuleni.

Kimsingi dhana ya Historia ya Tanzania na Maadili inajumuisha mfululizo wa matukio ya kihistoria yaliyotokea nchini na maadili yaliyojengwa tangu nyakati za kale hadi sasa. Tangu kale, jamii zetu zilikuwa zikisisitiza vitendo vya kimaadili vinavyosisitiza tabia za malezi bora kwa watoto na vijana, heshima, kuheshimiana, upendo, kujali watu wengine, ushirikiano, umoja na kupenda kufanya kazi kwa bidii. Vitendo hivi vilisitizwa kama msingi wa maendeleo katika jamii. Hata sasa, vitendo hivi vya kimaadili vinasisitizwa ili kukuza na kulinda maadili yetu. Hivyo, ni wajibu wetu kwa sasa kuendeleza vitendo vya maadili shuleni na nyumbani. Kujifunza Historia ya Tanzania na Maadili kutaisaidia jamii kwa sasa kujenga maadili, kukuza utaifa na kulinda maslahi ya nchi na rasilimali za Taifa. Kwa kufanya hivyo, tutaishi katika misingi ya utu, uadilifu, usawa, umoja na upendo.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 21 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Zoezi la jumla

Jibu maswali yafuatayo:

1. Eleza maana ya historia ya Tanzania.
2. Eleza umuhimu wa kujifunza historia ya Tanzania.
3. Jiulize, kisha andika hatua utakazochukua ikiwa:
   (a) Mwanafunzi mwenzako amejikwaa na kuanguka.
   (b) Mdogo wako analia.
   (c) Mtu mwenye ulemavu wa uoni yuko kandokando ya barabara akihitaji kuvuka.
   (d) Mwanafunzi mwenzako hana kalamu wakati wewe una kalamu mbili.
   (e) Mwanafunzi mwenzako anafanyiwa vitendo vya ukatili, unyanyasaji au udhalilishaji na mwanafunzi mwenzako.
   (f) Mwanafunzi mwenzako anafanyiwa vitendo vya ukatili, unyanyasaji au udhalilishaji na mtu aliyekuzidi umri.
   (g) Umeamka asubuhi na kukutana na watu waliokuzidi umri.
   (h) Umekutana na mwalimu amebeba daftari anaelekea darasani.
4. Andika **NDIYO** kwa sentensi inayoashiria kitendo cha rushwa na **HAPANA** kwa sentensi isiyoashiria kitendo cha rushwa.
   (a) Mwanafunzi amepiga kelele darasani lakini kiranja wa darasa hajaandika jina lake kwa vile ni ndugu au rafiki yake.
   (b) Mwalimu amempa alama za upendeleo mwanafunzi baada ya kupewa fedha na mzazi wa mwanafunzi huyo.
   (c) Mwanafunzi amechelewa kufika shuleni lakini hakuadhibiwa kwa vile kiranja alinunuliwa andazi na mwanafunzi huyo.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 22 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(d) Mlinzi nyumbani amepewa fedha ili auze mabati na saruji za ujenzi wa nyumba.
(e) Mwalimu kutoa majibu ya mtihani kwa wanafunzi kwa sababu walimpa zawadi siku yake ya kuzaliwa.

5. Eleza manufaa ya mtoto kuonywa na jamii anapokosea.
6. Taja faida nne za mtoto kuwa na tabia njema.
7. Eleza hasara za kuwa na tabia mbaya katika jamii.
8. Eleza misingi ya matendo ya kimaadili katika jamii za Kitanzania.
9. Andika mambo uliyojifunza kuhusu vitendo vya kimaadili.
10. Taja vyanzo sita (6) vya kupata taarifa za historia ya Tanzania.

Msamiati

Akiolojia taaluma ya uchunguzi wa kisayansi kuhusu masalia ya mambo ya kale na utamaduni wa mwanadamu

Anthropolojia taaluma inayohusu kusoma utamaduni wa historia ya maisha na maendeleo ya binadamu

Isimu historia hufafanunua taarifa za mabadiliko katika lugha kwa vipindi mbalimbali

Kuheshimiana kuoneshana tabia za adabu, kujali kwako na kwa watu wengine bila ubaguzi

Kushirikiana hali ya watu kuungana na kufanya jambo fulani kwa pamoja

Makumbusho maeneo yanayotumiwa kuhifadhi vitu vyenye historia na urithi wa kiasili na kiutamaduni

Tabia kitendo kinachofanyika mara kwa mara

Uhusiano hali ya kuwa na fungamano na wengine

Vitendo mambo yote yanayotendwa na binadamu

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 23 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Sura ya Pili

Urithi wa Tanzania

Utangulizi

Katika sura hii utajifunza dhana ya urithi na maeneo yenye urithi wa kihistoria nchini Tanzania. Pia, utajifunza wajibu wa jamii katika kulinda urithi wa kihistoria. Umahiri utakaoupata utakusaidia kuthamini urithi uliopo nchini na kutumia fursa zinazopatikana kutokana na urithi huu kwa maendeleo ya jamii.



Fikiri

Urithi uliopo Tanzania.

Maana ya Urithi

Kazi ya kufanya namba 1



Soma vyanzo mbalimbali, ikiwemo vitabu na mitandao, kuhusu maana ya neno urithi.

Urithi unajumuisha vitu vyenye thamani na kumbukumbu zilizohifadhiwa au kuwepo katika eneo fulani kutoka vizazi vilivyopita. Urithi huu unaweza kuwa ule unaoshikika kama vile, masalia ya binadamu wa kale, michoro ya mapangoni, magofu na masalia ya miji na majengo, vitu vya thamani kama shanga na zana zilizotumiwa na watu walioishi kale.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 24 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Urithi wa asili kama vile wanyama, milima, mito ya asili na maziwa ni sehemu ya urithi unaoshikika. Pia, urithi unaweza kuwa ule usioshikika kama vile mila, desturi, miiko, maarifa, dini na elimu ya jadi. Hivi vyote ni sehemu ya urithi kwani huonesha asili yetu, chimbuko letu au matukio yaliyotokea katika jamii zetu. Aidha, urithi umebeba utambulisho wa asili, tamaduni, mila na desturi zetu.

Maeneo yenye urithi unaoshikika

Tanzania ni nchi mojawapo duniani yenye urithi mwingi na adhimu unaoshikika.

Kazi ya kufanya namba 2



Tembelea maeneo yenye urithi kama vile magofu ya miji, misikiti, makanisa, masalia ya binadamu, zana za mawe, mbuga za wanyama, milima, mito ya asili na misitu katika maeneo unayoishi, kisha orodhesha urithi uliopo.

Masalia ya binadamu wa kale, michoro ya mapangoni, magofu na masalia ya miji na majengo, mbuga za wanyama, milima, mito ya asili, misitu na vitu vya thamani kama shanga na zana zilizotumiwa na watu walioishi kale ni sehemu ya urithi unaoshikika.

Urithi unaohusu binadamu wa kale na shughuli zake

Tanzania ina urithi adhimu kuhusu shughuli za binadamu wa kale na masalia yake. Mfano, Kondoa Irangi, Dodoma kuna kumbukumbu za michoro ya mapangoni yenye urithi wa kihistoria unaoonesha shughuli za jamii za kale (chunguza Kielelezo namba 1).

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 25 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Kielelezo namba 1: *Michoro ya mapangoni, Kondoa Irangi*

Eneo la Oldupai, Arusha ni mahali ambako kuligunduliwa masalia ya fuvu la binadamu wa kale. Mabaki haya yaligunduliwa na Dkt. Louis Leakey na Mary Leakey mwaka 1959. Huu ni urithi mkubwa kwa sababu inaaminika kuwa ndipo alipoishi binadamu wa kwanza duniani (chunguza Kielelezo namba 2).



Kielelezo namba 2: *Fuvu la binadamu aliyeishi kwa miaka mingi zaidi*

Pia, eneo la Laetoli, Arusha lina nyayo za binadamu anayeaminika kuishi kwa miaka mingi zaidi duniani (chunguza

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 26 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kielelezo namba 3). Huu ni urithi mkubwa kwa nchi yetu. Wageni huja nchini kutembelea maeneo hayo ili kujifunza historia ya watu wa kale.



Kielelezo namba 3: *Nyayo za binadamu wa kale, katika eneo la Laetoli*

Eneo la bonde la Isimila, Iringa kuna urithi wenye historia unaohusu Zana za Mawe zilizotumiwa na binadamu wa kale. Zana hizi za mawe zina mfanano na mikuki, mishale, shoka, visu na nyundo kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 4. Zana hizi zilitumika kuwinda, kuchimbia mizizi na kupondea vitu mbalimbali Urithi huu wa Zana za Mawe ni adhimu na muhimu kwa historia ya binadamu duniani.



Kielelezo namba 4: *Baadhi ya Zana za Mawe katika Makumbusho ya Isimila*

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 27 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Zoezi la 1.

1. Eleza kwa nini urithi huu uliopo eneo la Laetoli, Kondoa Irangi, Isimila na Oldupai ni muhimu?

Urithi wa kihistoria kuhusu wageni kutoka Mashariki ya Mbali na Kati

Jamii za Tanzania hapo Kale zilifanya biashara na wafanyabiashara kutoka Mashariki ya Mbali na ya Kati. Nchi hizo ni India, Irani, Iraki, Kuwait, China na Saud Arabia. Biashara hii ilifanyika katika miji iliyopo katika mwambao wa Pwani ya Bahari ya Hindi kama vile Dar es Salaam, Bagamoyo, Tanga, Kilwa na Zanzibar. Biashara hizi zilifanyika kwa kubadilishana bidhaa. Bidhaa kubwa katika biashara hii kutoka nchini ilikuwa dhahabu na pembe za ndovu. Dhahabu ilitoka Zimbabwe kupitia bandari ya Sofala, Msumbiji. Kutoka kwa wageni kuja nchini, bidhaa kubwa zilikuwa shanga na vyombo vya ndani kama vile mabakuli na sahani za udongo. Baadhi ya mabaki ya bidhaa hizi yapo katika Makumbusho hapa nchini, kama vile makumbusho ndogo iliyopo Kaole, Bagamoyo.

Biashara hizi zilisababisha wafanyabiashara hawa watajirike na kujenga miji, majengo, misikiti na makaburi. Majengo na miji hiyo kwa sasa vimebaki kama magofu na masalia yenye kumbukumbu ya kihistoria kuhusu wafanyabiashara hao. Kielelezo namba 5 kinaonesha mojawapo ya magofu ya mji uliotumiwa na wafanyabiashara hao.

FOR ONLINE USE ONLY

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 28 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Kielelezo namba 5: *Magofu ya mji wa Tongoni, Tanga*

Pia, eneo la Kunduchi lililopo Dar-es-salaam lina mabaki ya mji uliotumiwa na wafanyabiashara hao (chunguza Kielelezo namba 6).



Kielelezo namba 6: *Magofu ya mji wa Kunduchi, Dar es salaam*

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 29 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Vilevile, eneo la Kilwa, Lindi lina mabaki ya magofu ya mji, majengo na ikulu za viongozi waliojihusisha na biashara hii. Kilwa Kisiwani, ndio mji uliokuwa kituo muhimu na kikubwa wakati wa biashara zilizofanywa na watu kutoka Mashariki ya Kati. Kilwa kuna masalia ya jengo la mfalme wa Kilwa liitwalo Husuni Kubwa. Jumba hili lilikuwa ikulu ya sultani wa Kilwa (chunguza Kielelezo namba 7). Masalia haya yapo Kilwa, mkoa wa Lindi mpaka leo.



Kielelezo namba 7: *Magofu ya Husuni Kubwa, Kilwa*

Maeneo ya Kilwa kuna gofu la ngome ambalo lilijulikana kama ngome ya gereza. Ngome hii ilianza kujengwa na wageni kutoka Mashariki ya Kati, na baadae kumaliziwa kujengwa na Wareno kutoka Ulaya. Gofu la ngome hii nalo ni sehemu ya urithi nchini Tanzania (chunguza Kielelezo namba 8).

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 30 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Kielelezo namba 8: *Gofu la ngome ya gereza Kilwa, Lindi*

Vilevile, kuna urithi wa magofu ya misikiti iliyotumiwa na wafanyabiashara hao kwa ajili ya ibada. Jamii hizi zilishika dini ya Kiislamu. Miongoni mwa misikiti hii ipo Kilwa Kisiwani, Lindi na Kaole Bagamoyo, mkoa wa Pwani (angalia Kielelezo namba 9).



Kielelezo namba 9: *Gofu la msikiti mkuu Kilwa Kisiwani, Lindi*

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 31 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Pia, Kaole kuna magofu ya msikiti, makaburi na kisima kilichotumiwa na wafanyabiashara kutoka Mashariki ya Kati. Angalia magofu hayo katika Kielelezo namba 10.



Kielelezo namba 10: *Magofu yaliyopo Kaole, Bagamoyo*

Vilevile, Kaole kuna urithi wa bidhaa kama sahani na shanga zilizoletwa na wafanyabiashara kutoka Mashariki ya Mbali na Kati. Urithi wa bidhaa hizo upo katika makumbusho ndogo iliyopo Kaole. Makumbusho mbalimbali nchini zina bidhaa kama vile vigae, vyombo na shanga zilizoletwa na wafanyabiashara kutoka Mashariki ya Mbali na Kati.

Ushirikiano wa kibiashara baina ya wafanyabiashara kutoka Mashariki ya Mbali na Kati na jamii zetu ulisababisha kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili. Baadhi ya maneno ya lugha ya Kiswahili yamekopwa kutoka katika lugha zilizotumiwa na wafanyabiashara hao. Maneno kama vile, sadaka, mwalimu, akili, tisa, ahadi, shikamoo, marahaba, ahsante, madrasa na kitabu yamekopwa kutoka katika lugha ya Kiarabu. Pia, maneno

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 32 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kama gunia, dunia, pesa na gari yamekopwa kutoka katika lugha ya Kihindi. Haya ni baadhi tu ya maeneo tunayotumia katika lugha ya Kiswahili kwa sasa. Lugha ya Kiswahili ni urithi nchini.

Pia, jamii zilizoshirikiana na wafanyabiashara hao zimerithi tamaduni za kigeni kama vile dini ya Kiislamu, mavazi na maadili yao. Jamii hizi ni zile zilizopo hasa katika maeneo ya mwambao wa Pwani ya Bahari ya Hindi. Kielelezo namba 11 kinaonesha mfano wa mitindo ya mavazi hayo. Maadili haya ya kigeni yamekuwa sehemu ya urithi wa jamii zetu mpaka sasa.



Kielelezo namba 11: *Mitindo ya mavazi iliyoletwa na Waarabu*

Aidha, ujio wa wageni hao ulileta viungo mbalimbali vya chakula nchini kama vile mdalasini, iliki, pilipili manga, karafuu na binzari nyembamba kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 12.



Mdalasini



Iliki



Karafuu



Pilipili manga



Binzari nyembamba

Kielelezo namba 12: *Viungo vya chakula vilivyoletwa na wageni*

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 33 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Pia, baadhi ya mapishi ya vyakula kama vile pilau, jamii zetu zimerithi kutoka kwa wageni hao.

Kazi ya kufanya namba 3

Fanya uchunguzi maeneo ambayo wageni kutoka nchi za Mashariki ya Mbali na Kati walikaa, kisha andika maadili ambayo jamii hizo zimerithi.

Urithi wa Kihistoria unaohusu biashara ya utumwa nchini

Maeneo ya Bagamoyo kuna urithi wa magofu unaotokana na biashara ya utumwa. Wafanyabiashara wa biashara ya utumwa walitoka nchi za Uarabuni. Bagamoyo kuna jengo la Caravan Serai ambalo lilikuwa hoteli ya wafanyabiashara wa watumwa (chunguza Kielelezo namba 13).



Kielelezo namba 13: *Jumba la Caravan Serai, Bagamoyo*

Pia, maeneo ya Zanzibar kuna magofu na majengo yaliyotumiwa kwa ajili ya kuhifadhi watumwa na kuishi wafanyabiashara wa biashara ya watumwa (chunguza Kielelezo namba 14).

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 34 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Kielelezo namba 14: *Chumba cha chini kilichotumika kuweka watumwa, kilichopo eneo la kanisa la Anglikana Unguja, Zanzibar*

Urithi wa Kihistoria unaohusu wageni kutoka nchi za Ulaya

Tanzania ina urithi wa kihistoria ulioachwa na wageni waliokuja kutoka katika nchi za Ulaya. Baadhi ya wageni hawa walikuwa wamisionari. Awali, wageni hawa walikuja kueneza dini ya Kikristo. Hivyo, walijenga makanisa kadhaa katika maeneo waliyoishi. Ujio wa wageni hao uliacha urithi wa kihistoria wa makanisa yaliyojengwa kwa ajili ya ibada. Makanisa waliyoyajenga wamisionari hao bado yanatumika kwa ibada hadi sasa. Mfano wa makanisa hayo ni kanisa Katoliki la zamani lililopo Bagamoyo na kanisa la Anglikana lilipo Mkunazini, Zanzibar (chunguza Kielelezo namba 15).

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 35 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Kielelezo namba 15: *Kanisa la Anglikani, Zanzibar lililojengwa eneo la soko la watumwa*

Kuna makanisa mengine yaliyojengwa baadae wakati wa ukoloni hapa nchini. Mfano wa makanisa hayo ni Kanisa la Mtakatifu Yosefu na kanisa la Azania Front, yaliyopo Dar es Salaam. Pia, makanisa haya ni sehemu ya urithi wa kihistoria nchini kwa sasa. Licha ya urithi wa makanisa, wageni hawa walikuwa ndio chanzo cha kuingia Ukristo na maadili ya dini ya Kikristo nchini. Dini na maadili ya Kikristo ni sehemu ya urithi nchini hata leo.

Pia, tuna urithi wa mazao yaliyoletwa nchini na wageni kutoka nchi mbalimbali. Mazao hayo ni kama vile mahindi, maembe, viazi mviringo, mihogo na mapera. Mazao haya yanalimwa mpaka sasa na yamebaki kama sehemu ya urithi nchini.

Urithi uliopo katika makumbusho

Makumbusho ya Taifa yamehifadhi urithi wa kihistoria wa aina mbalimbali. Makumbusho haya ni; Kijiji cha Makumbusho

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 36 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kilichopo Kijitonyama, Dar es Salaam, Makumbusho ya Vita vya Majimaji, Songea mkoa wa Ruvuma, Makumbusho ya Azimio la Arusha, Arusha na Makumbusho ya Mwalimu Nyerere, Butiama mkoa wa Mara. Makumbusho mengine ni Makumbusho ya Elimu Viumbe, Arusha, Makumbusho na Nyumba ya Sanaa iliyopo Dar es Salaam na Makumbusho ya Kumbukumbu ya Rashidi Mfaume Kawawa iliyopo Songea. Pia, kuna makumbusho ya watu binafsi yenye taarifa za kihistoria kama vile makumbusho ya Bujora, Mwanza. Hizi ni baadhi za makumbusho nchini.

Kazi ya kufanya namba 4



Soma vyanzo mbalimbali ikiwemo tovuti na vitabu kuhusu Makumbusho yaliyopo nchini na eleza urithi uliopo kwenye makumbusho hayo.

Urithi wa asili

Tanzania ina urithi wa asili kama vile misitu, mbuga za wanyama, milima, mabonde, maziwa na mito.

Kazi ya kufanya namba 5



Fanya uchunguzi, kisha andika maeneo yenye urithi wa mbuga za wanyama, mito, mabonde, maziwa na milima kutoka katika mazingira unayoishi na taifa kwa ujumla.

Eneo la bonde la Isimila lililopo mkoani Iringa lina nguzo za asili zilizodumu kwa miaka mingi. Chunguza Kielelezo namba 16.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 37 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Kielelezo namba 16: *Nguzo za asili katika bonde la Isimila, Iringa*

Pia, Tanzania ina mbuga za wanyama kama vile Serengeti, Ngorongoro, Mikumi, Tarangire, Ruaha, Mkomazi, Udzungwa, Nyerere na Manyara ambazo ni urithi wa asili uliopo nchini. Angalia mfano katika Kielelezo namba 17.



Kielelezo namba 17: *Mbuga ya wanyama Ngorongoro, Arusha*

Hizi ni baadhi tu ya mbuga za wanyama zilizopo nchini. Wanyama waliopo katika mbuga hizi ni urithi wa asili uliopo Tanzania.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 38 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kazi ya kufanya namba 6

Fanya uchunguzi, kisha andika mbuga nyingine zilizopo nchini na baadhi ya wanyama waliopo katika mbuga hizo.

Vilevile, kuna milima mikubwa nchini ambayo ni urithi wa asili. Mfano wa milima hiyo ni mlima Kilimanjaro, ambao ndio mlima wa kwanza kwa urefu barani Afrika (chunguza Kielelezo namba 18). Kuna milima mingine ambayo ni urithi wa asili, kama vile mlima Meru, milima ya Udzungwa na mlima Rungwe.

Kazi ya kufanya namba 7

Fanya uchunguzi na andika milima mingine zaidi ambayo ni urithi wa asili nchini.



Kielelezo namba 18: *Mlima Kilimanjaro*

Tanzania kuna maziwa na mito ya asili ambayo ni alama ya urithi nchini. Baadhi ya maziwa yaliyopo nchini ni ziwa Victoria, ziwa Tanganyika, ziwa Manyara, na ziwa Nyasa. Pia, kuna mito mikubwa ya asili mfano, mto Ruaha, Kilombero, Malagarasi, Rufiji, Wami na Ruvuma. Hii ni baadhi ya mito mikubwa ya asili ambayo ni urithi wa asili nchini. Vilevile, misitu na uoto wa asili ni sehemu ya urithi nchini.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 39 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kazi ya kufanya namba 8

Fanya uchunguzi na orodhesha mito na maziwa mengine ambayo ni urithi wa asili nchini.

Urithi usioshikika

Urithi usioshikika unahusu masuala ya kijamii yaliyorithiwa kutoka kizazi hadi kizazi ambayo hayawezi kuonekana au kushikika. Urithi huu unahusisha masimulizi kama vile hadithi, miiko, ngano, nyimbo, midundo ya ngoma, methali na lugha za asili. Pia, unahusisha shughuli za kijamii kama vile matambiko, dini na matamasha ya jadi. Vilevile, unahusu maarifa ya jadi kuhusu kilimo, uvuvi, uhunzi, ufugaji na elimu ya mazingira. Sanaa za maonesho kama vile maigizo na tafsiri za sanaa za ufundi kama vile uchoraji na uchongaji ni sehemu ya urithi usioshikika (angalia mfano katika Kielelezo namba 19). Vitu hivi kwa pamoja ni mfano wa urithi usioshikika wenye kubeba mila, desturi, maarifa na ujuzi wa asili wa jamii za kale.



Kielelezo namba 19: *Uchongaji wa vinyago vyenye tafsiri mbalimbali*

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 40 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kazi ya kufanya namba 9



Fanya uchunguzi na andika urithi usioshikika uliopo katika maeneo yanayokuzunguka.

Urithi uliopo nchini kwa ujumla ni maarufu kwa utalii kwa sasa. Wageni wengi kutoka nje na ndani ya nchi huenda kutembelea urithi huu.

Umuhimu wa urithi katika taifa

Urithi una umuhimu kwa jamii na Taifa kwa ujumla. Urithi huu ni muhimu katika:

(a) Kutambulisha urithi uliopo nchini;

(b) Kutupa ushahidi wa chimbuko na asili za jamii na maadili yake;

(c) Kupata historia ya jamii zetu;

(d) Kutambulisha maarifa na ujuzi wa asili wa jamii za Kitanzania;

(e) Kutoa ufahamu juu ya asili na mabadiliko ya jamii za Kitanzania;

(f) Kuchochea maendeleo ya kiuchumi kupitia utalii;

(g) Kutoa ushahidi wa chimbuko la tamaduni zetu;

(h) Kupata taarifa za mabadiliko ya jamii na jinsi ya kuyaendeleza; na

(i) Kupata pato la Taifa kwa njia ya utalii.

Kazi za kufanya namba 10



Andika mambo uliyojifunza kuhusu urithi wa kihistoria.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 41 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Wajibu wa jamii katika kutunza maeneo ya urithi wa Tanzania

Kazi ya kufanya namba 11



Fanya uchunguzi na kisha andika urithi uliopo katika maeneo ya karibu na andaa mpango wa kutunza na kulinda urithi huo.

Maeneo yenye urithi yanapaswa kuhifadhiwa na kuthaminiwa. Jamii ya Kitanzania ndiyo yenye wajibu wa kutunza maeneo haya. Maeneo yenye urithi yanapaswa kutunzwa na kulindwa kwa kufanya mambo yafuatayo:

(a) Kuhifadhi kumbukumbu halisi ya wakati, eneo, na matumizi ya urithi huo;

(b) Kufanya usafi na ukarabati ili kuzuia uharibifu wa urithi uliopo;

(c) Kuheshimu ubunifu wa miundo, aina na mbinu wakati wa ujenzi ili kuendeleza uhalisi wa urithi uliopo; na

(d) Kuweka mandhari ya mazingira salama ili kuzuia uharibifu.

Zoezi la jumla

1. Andika neno **NDIYO** mbele ya sentensi ambayo ni kweli na neno **HAPANA** mbele ya sentensi ambayo si kweli.
   (i) Makanisa yenye urithi wa historia hayatumiki kwa sasa.
   (ii) Kilwa ulikuwa mji maarufu kwa biashara ya watumwa.
   (iii) Bagamoyo na Zanzibar ilikuwa miji iliyohusika na biashara ya utumwa.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 42 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iv) Magofu ya mji wa Kunduchi yalijengwa wakati wa biashara kati ya jamii zetu na nchi za Mashariki ya Mbali na Kati.

(v) Maadili ya jamii za mwambao wa Bahari ya Hindi yamechangiwa na wafanyabiashara kutoka Mashariki ya Mbali na Kati.

2. Oanisha kipengele kutoka sehemu **A** na maeneo yaliyopo sehemu **B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi katika sehemu uliyopewa.

Sehemu A	**Jibu**	**Sehemu B**
(i) Jumba la wafanyabiashara ya utumwa		A. Kilwa Kisiwani, Kaole
(ii) Makumbusho ya Vita vya Majimaji		B. Husuni Kubwa
(iii) Maeneo yenye historia ya watumwa		C. Oldupai
(iv) Maarufu kwa michoro ya mapangoni		D. Bagamoyo na Zanzibar
(v) Makanisa yanayotumika ambayo ni urithi wa Tanzania		E. Kilwa, Tongoni, Pangani na Kunduchi
(vi) Eneo lenye magofu na masalia yenye miji iliyotumiwa na wafanyabiashara kutoka Mashariki ya Mbali na Kati		F. Laetoli

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 43 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(vii) Gofu la ikulu ya sultani wa Kilwa		G. Tanga
(viii) Urithi wa misikiti ya kale		H. Kondoa Irangi
(ix) Kuligundulika binadamu wa kale zaidi		I. Anglikani Mkunazini, Zanzibar, Azania Front
(x) Kuna nyayo za binadamu wa kale		J. Caravan Serai
		K. Songea

3. Andika umuhimu wa urithi wa Tanzania.
4. Andika mambo uliyojifunza kuhusu urithi uliopo nchini.
5. Andika urithi wa kimaadili na kitamaduni tuliorithi kutoka kwa wageni waliokuja nchini.

Msamiati

Husuni jumba lililotumiwa na wafalme au sultani kama makazi

Kale huhusisha zamani au miaka mingi iliyopita

Maadili tabia, mienendo, kanuni, nidhamu za jamii husika

Magofu mabaki ya majengo ya kale yanayoonekana

Makumbusho maeneo yenye kuhifadhi vitu vyenye urithi wa kiasili na kiutamaduni

Oldupai eneo hili hujulikana pia kama bonde la olduvai

Sultani ni mfalme au mtawala wa nchi, jina lilitumiwa na watawala wa Kiarabu

Utumwa mfumo ambao binadamu alitumikishwa bila malipo na kumilikiwa na mtu mwingine. Mtumwa hana uhuru wa mali, hata watoto walikuwa ni mali ya aliyemmiliki.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 44 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Sura ya Tatu

Wajibu na haki za mtoto

Utangulizi

Katika sura hii utajifunza kuhusu wajibu wa mtoto katika familia na shuleni. Pia, utajifunza kuhusu haki za mtoto katika familia na shuleni. Umahiri utakaoupata katika sura hii utakuwezesha kutambua haki zako na wajibu wako. Pia, utakuwezesha kutekeleza wajibu wako nyumbani na shuleni.



Fikiri

Haki na wajibu wa mtoto.

Wajibu wa mtoto

Kazi ya kufanya namba 1



Andika mambo unayofanya nyumbani na shuleni.

Mambo tunayotakiwa kufanya shuleni na nyumbani ni wajibu wetu. Wajibu ni jambo au mambo ambayo mtu anapaswa kuyafanya au kuyatimiza. Wajibu mara nyingi ni mambo unayowajibika kuyafanya au kitu unachotarajiwa kukifanya ili kuendana na taratibu na kanuni za kimaadili zilizopo katika mazingira unayoishi, shuleni au nyumbani.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 45 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Soma matendo mchanganyiko katika sehemu A, kisha fanya zoezi linalofuata.

Sehemu A **Matendo mchanganyiko**	**Sehemu B**	**Sehemu C**
Kufanya usafi darasani, kuwaheshimu wakubwa na wadogo, kununua chakula, kuwasalimia wazazi, kuwahi kurudi nyumbani, kununua kalamu, kuwasaidia wazee, kufanya usafi wa mwili, kutii sheria za shule, kununua mavazi, kuwatii wazazi, kuosha vyombo unavyolia chakula, kufua nguo zako, kuwatii walimu, kuhudhuria vipindi darasani, kumaliza kazi za shule na darasani		

Zoezi la 1

1. Andika matendo yanayoonesha wajibu katika sehemu B na matendo ambayo siyo wajibu katika sehemu C.
2. Eleza kwa nini matendo uliyoorodhesha katika sehemu B ni wajibu wa mtoto.
3. Eleza kwa nini matendo uliyoorodhesha katika sehemu C siyo wajibu wa mtoto.

Kielelezo namba 1 kinaonesha baadhi ya wajibu wa mtoto.



Kielelezo namba 1: *Wajibu wa mtoto*

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 46 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Wajibu wa mtoto shuleni

Watoto wanatakiwa kutimiza wajibu wao wakiwa shuleni.

Kazi ya kufanya namba 2



Fikiri na andika wajibu wako shuleni.

Mambo unayolazimika kuyafanya shuleni ili kuendana na taratibu, kanuni na sheria za shule ni wajibu wako kama mwanafunzi. Ni wajibu wa mtoto kwa sababu ni vitendo vya kimaadili anavyopaswa kufanya mtoto anapokuwa shuleni. Mfano wa wajibu wa mtoto shuleni ni pamoja na:

(a) Kuwahi shuleni na kuwepo darasani kwa wakati sahihi (chunguza Kielelezo namba 2);



Kielelezo namba 2. *Watoto wakielekea shuleni*

(b) Kusoma kwa bidii na kufanya kazi zote zinazohusu masomo;
(c) Kushirikiana na wanafunzi wengine shuleni;
(d) kutii sheria za shule;
(e) Kujilinda na kulinda wanafunzi wengine dhidi ya vitendo vya ukatili, udhalilishaji na unyanyasaji shuleni;

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 47 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(f) Kuthamini mali za shule na kuepuka vitendo vya rushwa vinavyolenga kuharibu na kupoteza mali za shule;
(g) Kutoa taarifa zinazohusu uharibifu na upotevu wa mali za shule;
(h) Kuwapenda wanafunzi wenzake na watu wengine shuleni;
(i) Kuwasaidia walimu, watu waliokuzidi umri na wanafunzi wengine shuleni pale inapohitajika;
(j) Kuwatii walimu, viongozi na wafanyakazi wengine waliopo shuleni;
(k) Kuwaheshimu walimu, waliokuzidi umri na wanafunzi wengine; na
(l) Kufanya usafi wa mazingira ya shule na darasani (chunguza Kielelezo namba 3).



Kielelezo namba 3: *Wanafunzi wakifanya usafi maeneo ya shule*

Kuacha kutimiza wajibu wako shuleni ni kinyume na vitendo vya kimaadili. Unapaswa kutambua kuwa kutimiza wajibu ni jambo la lazima uwapo shuleni.

Kazi ya kufanya namba 3

Andika mambo mengine ambayo ni wajibu wako shuleni.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 48 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Wajibu wa mtoto nyumbani

Watoto wanatakiwa kutimiza wajibu wao wakiwa nyumbani ili kuwa na tabia za kimaadili.

Kazi ya kufanya namba 4

Fikiri na andika wajibu wako nyumbani.

Mambo unayopaswa kuyafanya nyumbani ili kuendana na taratibu na kanuni za kimaadili ni wajibu wako kama mtoto. Mfano wa wajibu wa mtoto nyumbani ni pamoja na:

(a) Kuwaheshimu wazazi, walezi, watu waliokuzidi umri na watoto wenzako;
(b) Kufanya kazi za nyumbani zinazolingana na umri wake;
(c) Kuthamini mali zako binafsi na za nyumbani;
(d) Kuepuka vitendo vya rushwa vinavyolenga kutenda vitendo vilivyo kinyume na maadili;
(e) Kuwasaidia wazazi, walezi na watu waliokuzidi umri kufanya kazi kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 4;



Kielelezo namba 4: *Watoto wakifanya kazi kwenye bustani*

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 49 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(f) Kutenda vitendo vya kimaadili vinavyokubalika na jamii yako;

(g) Kujilinda na kulinda watoto wengine dhidi ya vitendo vya ukatili, udhalilishaji na unyanyasaji maeneo ya nyumbani;

(h) Kuwasadia wadogo zako wanapohitaji msaada kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 5;



Kielelezo namba 5: *Kaka akimsaidia mdogo wake kuvaa nguo*

(i) Kufanya usafi binafsi wa mwili, nguo na vyombo ulivyotumia kula chakula kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 6; na



Kielelezo namba 6: Mtoto akifanya usafi wa vyombo alivyolia chakula

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 50 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(j) Kuacha kuiga vitendo vilivyo kinyume na maadili ya jamii yetu ili kujenga maadili yanayofaa nchini.

Kazi ya kufanya namba 5



Andika wajibu wako mwingine unaopaswa kutimiza ukiwa nyumbani.

Umuhimu wa kutimiza wajibu

Kitendo cha kuacha kutimiza wajibu wako nyumbani ni kukosa maadili. Unapaswa kutambua kuwa kutimiza wajibu ni jambo la lazima uwapo nyumbani.

Kazi ya kufanya namba 6



Fikiri na eleza umuhimu wa kutimiza wajibu shuleni na nyumbani.

Kutimiza wajibu ni jambo muhimu katika maisha ya kila siku. Mtu anayetimiza wajibu anatekeleza mambo anayotakiwa kufanya kwa ufanisi. Kutimiza wajibu huleta hali ya ufanisi katika kazi na huwezesha kufikia lengo. Kutimiza wajibu wako shuleni na nyumbani kutakusaidia:

(a) Kujenga uhusiano mzuri na watu wanaokuzunguka shuleni na nyumbani;

(b) Kujilinda na kulinda watoto na watu wengine dhidi ya vitendo vya ukatili, unyanyasaji na udhalilishaji;

(c) kufikia malengo uliyojiwekea na yaliyowekwa shuleni na nyumbani kwa wakati na kwa ufanisi;

(d) Kujenga uaminifu kati yako na wazazi, walimu na watoto wenzako;

(e) kupendwa na wazazi, walezi na wanafunzi wenzako;

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 51 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(f) Kutii sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa nyumbani na shuleni; na

(g) Kuonesha heshima na upendo kwa watu wengine unaoishi nao.

Haki za mtoto

Haki ni jambo au kitu chochote unachostahili kuwa nacho kama mtoto au kupokea kutoka kwa watu wengine kwa mujibu wa sheria. Pia, haki ni kile unachoruhusiwa kufanya kama mtoto. Haki za mtoto hutolewa na wazazi, walezi, walimu na watu wote katika jamii. Angalia baadhi ya haki za mtoto katika Kielelezo namba 7.

Kazi ya kufanya namba 7

Tafuta mambo yanayohusu haki za mtoto kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo vitabu, tovuti, na maktaba mtandao.



Kielelezo namba 7: *Haki za mtoto*

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 52 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Haki za mtoto ni pamoja na:

(a) Kuheshimiwa na kuthaminiwa kama watu wengine;

(b) Kuishi na wazazi na walezi wake bila kubaguliwa;

(c) Kupatiwa mahitaji yake muhimu kama vile chakula, huduma za afya, mavazi na malazi kwa ajili ya ustawi wake;

(d) Kutoa maoni, mawazo, kusikilizwa na kutoa uamuzi wa ustawi wake;

(e) Kupata jina na utaifa wake;

(f) Kutoajiriwa katika ajira za aina yoyote;

(g) Kunufaika na kutumia kwa uangalifu mali za wazazi wake;

(h) Kwenda shule na kupata elimu bora kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 8;



Kielelezo namba 8: *Watoto wakiaga wazazi tayari kwenda shuleni*

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 53 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(i) Kupata nafasi ya kushiriki katika michezo na shughuli za kiutamaduni kama ilivyo katika Kielelezo namba 9;



Kielelezo namba 9: *Watoto wakicheza michezo mbalimbali*

(j) Kusikilizwa na kupata msaada pale unapohitajika kama ilivyo katika Kielelezo namba 10;



Kielelezo namba 10: *Mwalimu akimsikiliza na kumsaidia mwanafunzi*

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 54 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(k) Kulindwa dhidi ya ukatili, udhalilishaji na unyanyasaji wa aina yoyote; na

(l) Kutoa taarifa iwapo atatendewa vitendo vya ukatili, udhalilishaji na unyanyasaji na wazazi, walezi au mtu yeyote unayemwamini. Pia, anaweza kutoa taarifa kwa walimu au vyombo vya usalama kama vile polisi au ofisi za kata, kijiji au mtaa kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 11.



Kielelezo namba 11: *Mtoto akitoa taarifa kituo cha polisi*

Kazi za kufanya namba 8

Chunguza na andika vitendo ambavyo ni kinyume na haki za mtoto vinavyofanyika maeneo ya shuleni na nyumbani.

Kuna vitendo vinavyofanyika katika mazingira ya shule na nyumbani ambavyo ni kinyume na haki za mtoto. Mtoto ana haki ya kulindwa dhidi ya ukatili, udhalilishaji na unyanyasaji wa aina yoyote. Mtoto ana haki ya kusema, kutoa taarifa na kupigania haki zake mwenyewe anapotendewa vitendo vilivyo kinyume na haki zake.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 55 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kimsingi haki za mtoto zinaambatana na wajibu ambao watu wazima kama vile wazazi, walezi na walimu wanatakiwa kutimiza kwa mtoto. Wajibu huo unaweza kulenga katika mahitaji ya mtoto ya kimwili, kielimu, kiulinzi au kiafya. Haki za mtoto ni za lazima kwake. Hii ni kwa sababu mtoto ni binadamu kama watu wengine na ana haki sawa.

Wajibu katika kusimamia na kulinda haki za mtoto

Mtoto anastahili kulindwa dhidi ya vitendo vya ukatili, unyanyasaji na udhalilishaji katika maeneo yanayomzunguka. Jamii inapaswa kuepuka vitendo vya ukiukwaji wa haki za mtoto.

Kazi ya kufanya namba 9



Fikiri na eleza jinsi ya kulinda haki za mtoto shuleni na nyumbani.

Haki za mtoto zinaweza kulindwa kwa kufanya mambo yafuatayo:

(a) Kuiwezesha jamii kutambua haki za mtoto;
(b) Kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kulinda haki za mtoto;
(c) Kuwaelimisha wazazi, walezi na jamii kuhusu athari za vitendo vya ukatili, udhalilishaji na unyanyasaji wa watoto;
(d) Kutoa adhabu kali kwa wote wanaokiuka haki za mtoto;
(e) Kutoa taarifa katika mamlaka mbalimbali inapotokea ukiukaji wa haki za mtoto;
(f) Kuelimisha watoto kuhusu haki zao;
(g) Kuelimisha watoto maeneo ya kutoa taarifa pale wanapotendewa vitendo vya ukiukaji wa haki zao;

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 56 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(h) Kushirikiana katika jamii kulinda haki za mtoto; na

(i) Kuwajengea watoto ujasiri wa kusema na kutoa taarifa pale wanapotendewa ukatili, udhalilishaji na unyanyasaji.

Ni wajibu wa jamii na watoto wenyewe kusimamia na kulinda haki za mtoto. Pia, ni muhimu jamii nzima kuwajibika katika kuhakikisha haki za mtoto katika maeneo ya shule na nyumbani zinaheshimiwa. Kuheshimu haki za mtoto kutasaidia kumpa nafasi mtoto ya kutimiza ndoto zake katika maisha.

Zoezi la jumla

1. Chunguza matendo katika jedwali yanayohusu haki na wajibu wa mtoto. Weka alama ya (✓) kwenye kisanduku kwa kubainisha matendo ya haki na wajibu wa mtoto. Angalia mfano namba 1 na 2.

Na	Matendo	Haki	Wajibu
i.	Kuwasalimia watoto wengine na watu waliokuzidi umri		✓
ii.	Kupata mahitaji ya shule, chakula na malazi	✓	
iii.	Kushirikishwa kufanya maamuzi		
iv.	Kuwathamini watu wenye mahitaji maalumu		
v.	Kupata nafasi ya kucheza		
vi.	Kupata malezi bora		
vii.	kuheshimiwa na watu wengine		
viii.	Kulindwa		
ix.	Kufanya kazi zinazolingana na uwezo wa mtoto		
x.	Kupata elimu bora		

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 57 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Chagua jibu sahihi na kuandika herufi ya jibu hilo katika sehemu iliyoachwa wazi.
   (i) Vitendo vifuatavyo vinaonesha ukiukwaji wa haki za mtoto isipokuwa _____
      (a) kupewa adhabu pale mtoto anapofanya kosa
      (b) kunyimwa chakula kama adhabu
      (c) kuajiriwa katika ajira ndogondogo
      (d) kupigwa maeneo ya kichwa, mgogo na miguu
   (ii) Matendo gani kati ya haya si wajibu wa mtoto ____
      (a) kufanya usafi binafsi wa mwili na nguo zake
      (b) kutafuta fedha za chakula cha familia nyumbani
      (c) kufanya usafi mahali anapolia chakula
      (d) kusaidia wazazi na walezi kufanya kazi mbalimbali
   (iii) Zifuatazo ni haki za mtoto isipokuwa_____
      (a) kupata elimu bora
      (b) kuheshimiwa kama watu wengine
      (c) kupata nafasi ya kucheza
      (d) kutosikilizwa anapohitaji msaada

Msamiati

Udhalilishaji kufanyiwa matendo ya kuabishwa

Ukatili matendo ya kuumiza, hali ya mateso, maumivu dhidi ya mtu mwingine kwa makusudi

Unyanyasaji matendo ya kuachwa, kudharauliwa au watu kutokujali kwa makusudi

FOR ONLINE USE ONLY

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 58 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Sura ya Nne

Matendo ya kuthamini maadili

Utangulizi

Katika sura hii utajifunza matendo ya kuthamini maadili kama kuheshimu wengine, kutii sheria na kujithamini. Pia, utajifunza matendo ya kujali na kushirikiana na watu wengine nyumbani na shuleni. Umahiri utakaoupata utakuwezesha kujenga uhusiano mzuri na watu wengine katika jamii inayokuzunguka kwa kutenda matendo ya kimaadili.



Fikiri

Matendo yanayoonesha kuthamini maadili.

Kuthamini maadili ni hali ya kuonesha mwenendo mzuri kwa kutenda matendo yanayokubalika katika jamii husika. Kuthamini maadili hutuwezesha kujenga uhusiano mzuri na watu wengine katika jamii inayotuzunguka, shuleni na nyumbani.

Kuheshimu watu wengine

Kutenda matendo ya kuheshimu watu wengine ni kitendo cha kuthamini maadili. Matendo ya kuheshimu watu wengine yanaweza kufanywa kwa ama kwa kuonesha utii, kusalimia, kusaidia kazi au kujali watu wengine.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 59 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Soma matendo yafuatayo, kisha fanya zoezi linalofuata.

(a) Mtoto kuwasalimia walimu na wenzake shuleni.

(b) Mtoto anamsaidia mwalimu kubeba madaftari kupeleka ofisini.

(c) Mwanafunzi anamsaidia mwalimu kufuta ubao.

(d) Mtoto anakataa kutumwa dukani na mama yake.

(e) Mtoto anamwita mama yake kwa jina lake.

Zoezi la 1

1. Matendo gani yanaonesha heshima na kwa nini?
2. Matendo gani yanaonesha kukosa heshima na kwa nini?
3. Taja matendo mengine yanayoonesha heshima kwa watu wengine.
4. Taja matendo mengine yanayoonesha kukosa heshima kwa watu wengine.

Kutii sheria

Sheria ni taratibu na kanuni zilizowekwa katika mazingira tuliyopo, shuleni, nyumbani au katika jamii, na hupaswa kufuatwa na kila mtu. Utii wa sheria ni jambo linalosisitizwa katika jamii zetu. Tangu zamani mtu aliyevunja sheria aliadhibiwa adhabu kali. Mfano, mtu ambaye alivunja sheria aliweza kuchapwa viboko hadharani.

Kuthamini utii wa sheria shuleni

Unapaswa kuonesha utii wa sheria za shule kwa kufuata taratibu na kanuni zilizopo shuleni. Baadhi ya sheria hizo ni kuwahi shuleni na kuhudhuria masomo kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 1.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 60 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Kielelezo namba 1: *Mwanafunzi akikimbia kuwahi shuleni*

Kufanya na kumaliza kazi zote zinazohusiana na masomo unapokuwa darasani, kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 2, ni kuonesha matendo ya kuthamini sheria shuleni.



Kielelezo namba 2: *Wanafunzi wakifanya kazi darasani*

Aidha, kuwatii walimu, watu waliokuzidi umri na kutopigana na wenzako kunaonesha kuthamini utii wa sheria shuleni.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 61 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kazi ya kufanya namba 1



Andika vitendo vingine vinavyoonesha kuthamini utii wa sheria shuleni.

Kutokutii sheria za shule ni kinyume na maadili. Hivyo, mwanafunzi asiyetii sheria za shule hupewa adhabu. Utii wa sheria shuleni huweka mazingira salama kwa ajili ya wanafunzi wote kusoma. Ni muhimu kutii sheria za shule ili uweze kujifunza katika mazingira salama shuleni.

Kuthamini utii wa sheria nyumbani

Kama ilivyo shuleni, nyumbani kuna kanuni na taratibu zake. Pia, kama watoto, ni muhimu kutii sheria zilizopo nyumbani kama vile, kuwahi kurudi nyumbani na kufanya kazi zote tunazopaswa kufanya nyumbani.

Kazi za kufanya namba 2



Andika vitendo vingine vinavyoonesha kuthamini utii wa sheria nyumbani.

Kutii sheria zilizopo nyumbani huongeza upendo kati ya watoto na wazazi wao.

Kuthamini utii wa sheria barabarani

Utii wa sheria za usalama wa barabarani ni muhimu. Sheria za usalama wa barabarani zinajumuisha alama, kanuni na taratibu za kufuatwa na watumiaji wa barabara. Sheria hizi huwasaidia watumiaji wa barabara kujua namna ya kutumia barabara. Tunapaswa kutii na kuheshimu sheria za barabarani ili kuepuka kupata ajali au kusababisha ajali za barabarani. Ni muhimu kuzijua na kuzifuata alama za barabarani ili kulinda maisha yako na ya watu wengine.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 62 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Zoezi la 2

1. Taja alama za barabarani unazozifahamu.
2. Eleza maana ya alama za barabarani unazozifahamu.

Kuna alama za barabarani ambazo zinazotoa ishara kwa watu wanaotembea kwa miguu kuvuka barabara (chunguza Kielelezo namba 3).



Kielelezo namba 3: *Alama za barabarani kwa wanaovuka kwa miguu*

Alama hizo ni alama ya pundamilia. Alama hii huchorwa katika barabara kwa rangi nyeupe. Ni vema kupita sehemu hiyo unapotaka kuvuka barabara. Pia, kuna taa za barabarani zinazoonesha ishara wakati wa kuvuka barabara. Alama hii ina alama ya mtu akitembea kwa haraka. Tunapoona alama hii tunapaswa kuvuka barabara kwa haraka endapo ni salama.

Pamoja na alama hizi, tunapaswa kuwa makini tunapovuka barabara. Toa ishara kwa mwendesha gari iwapo anakuja kwa mwendo wa kasi. Hakikisha unapovuka kuna taa nyekundu inayowaka kuashiria magari kusimama. Epuka kuvuka barabara wakati taa ya kijani inawaka kuruhusu magari kupita, hata kama kuna alama ya pundamilia. Tambua kuwa kuna madereva wa magari wazembe wasiozingatia alama hizi za barabarani.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 63 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kazi ya kufanya namba 3



Orodhesha mambo uliyojifunza kuhusu utii wa sheria za usalama wa barabarani.

Kujithamini

Kazi ya kufanya namba 4



Fikiri na andika matendo ya kuonesha kujithamini.

Matendo tuliyoandika yanaonesha kujithamini. Kujithamini huhusisha kujipenda wewe mwenyewe na kuwapenda watu wengine. Tunapoonesha kuwapenda watu wengine bila kujali hali zao ni dalili za kujithamini sisi pia. Hatuwezi kujithamini iwapo hatuwathamini watu wengine. Baadhi ya matendo ya kujithamini ni kujijali, kujiheshimu na kujikinga na mambo yatakayokuletea madhara.

Kazi ya kufanya namba 5



Onesha matendo ya kujithamini darasani.

Matendo ya kujithamini hujenga maadili ya jamii yako. Hii ni kwa sababu hutujengea heshima na uhusiano mzuri na watu wengine.

Zoezi la 3

1. Andika iwapo matendo haya ni ya kujithamini au si ya kujithamini
   (a) Mtoto anakataa kufua nguo zake.
   (b) Mtoto anaoga kabla ya kwenda shuleni.
   (c) Mtoto hakuchana nywele zake.
   (d) Mtoto anavaa sweta anapohisi baridi.
   (e) Mtoto amevaa nguo safi.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 64 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Chunguza picha katika Kielelezo kifuatacho, kisha fanya zoezi linalofuata.

A.



B.



C.



D.



Kielelezo namba 4: *Matendo ya kujithamini*

Zoezi la 4

1. Eleza ulichojifunza kutokana na picha A, B, C na D.
2. Eleza jinsi matendo yaliyopo katika picha A, B, C na D yanavyoweza kukusaidia katika maisha yako ya kila siku.
3. Andika mambo mengine yanayoonesha matendo ya kujithamini.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 65 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kuwajali watu wengine

Kujali watu wengine ni matendo ya kuthamini maadili ya jamii za Kitanzania.

Kazi ya kufanya namba 6

Soma taarifa zifuatazo na eleza matendo utakayofanya.

1. Ukikutana na mzee amebeba mzigo.
2. Rafiki yako akiumia wakati mnacheza mpira.
3. Ukiokota begi la shule la mwanafunzi mwenzako.
4. Ukipata taarifa mwanafunzi mwenzako amelazwa hospitalini.
5. Mwanafunzi mwenzako anafanyiwa vitendo vya ukatili na watu wengine.

Kusaidia watu wengine, kama vile, wazee, wagonjwa na watu wenye ulemavu ni kuonesha matendo ya kujali watu wengine (chunguza Kielelezo namba 5).



Kielelezo namba 5: *Matendo ya kuwajali watu wengine*

Zoezi la 5

1. Eleza matendo mengine yanayoonesha kuwajali watu wengine yanayofanyika shuleni na nyumbani.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 66 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Unapotenda matendo mema kwa mwenzako inaonesha jinsi unavyomjali. Kumjali mtu mwingine ni kumtendea jambo kwa namna ambayo wewe ungependa kutendewa. Matendo ya kuwajali wengine ni kuwapenda, kuwaheshimu na kuwasaidia. Pia, kutoa taarifa kwa walimu, wazazi, walezi au polisi kuhusu vitendo vya ukatili, udhalilishaji au unyanyasaji vinavyofanywa dhidi ya wanafunzi na watoto wengine ni matendo ya kuwajali watu wengine. Kuwajali wengine ni kitendo cha kuwakinga watu wengine dhidi ya mambo yatakayoweza kuwaletea madhara.

Kushirikiana na watu wengine

Matendo ya kushirikiana na watu wengine huonesha kuthamini maadili.

Kazi ya kufanya namba 7

Orodhesha matendo matatu mnayoyafanya pamoja na wenzako.

Chunguza picha zifuatazo katika Kielelezo namba 6, kisha fanya zoezi linalofuata.

A.



Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 67 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

B.



C.



Kielelezo namba 6: *Matendo ya ushirikiano*

Zoezi la 6

1. Eleza matendo yanayofanyika katika Kielelezo A, B, na C.
2. Eleza faida ya kutenda matendo yaliyopo katika Kielelezo A, B, na C.

Ushirikiano ni matendo ya kufanya kazi pamoja. Watu wanaoshirikiana hufanya kazi pamoja ili kupata ufanisi wa pamoja bila ya ushindani kati yao kwa manufaa binafsi. Ushirikiano mzuri hujengwa kwa kuwasiliana vyema na wenzako. Watu wanaowasiliana vizuri wanatumia lugha ya upole, ambayo si ya maneno ya kejeli wala matusi. Pia, kuwasiliana vizuri kunafanyika kwa kusikiliza wenzetu na kutokatisha mazungumzo yao wakati wanapoongea.

Ushirikiano ni hali ya kuthamini maadili yetu. Tangu kale, jamii zetu zilishirikiana katika shughuli za kijamii kama sherehe na msiba. Pia, jamii zilishirikiana katika shughuli za uchumi kama vile kilimo, biashara, ufugaji, uvuvi na ujenzi wa nyumba. Ushirikiano ulisaidia kutatua matatizo kwa pamoja na kujenga uhusiano mzuri. Pia, ushirikiano ulisababisha watu wapendane na kuishi pamoja. Hata sasa ushirikiano unaweza kufanyika kati ya mtu na mtu au kikundi kimoja

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 68 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

na kingine. Pia, unaweza kufanyika kati ya shule na shule. Ushirikiano shuleni unaweza kufanyika zaidi katika masuala ya kitaaluma, kiutamaduni, michezo na masuala mengine ya shule kwa kufanya kazi pamoja.

Kazi ya kufanya namba 8



Fanya uchunguzi na andika mambo ambayo watu wa mtaa au kijiji chako hufanya kwa ushirikiano.

Tunaweza kushirikiana na majirani zetu katika mitaa na vijiji. Jamii zetu zinaweza kushirikiana katika kazi za ujenzi wa shule na barabara, kazi za kilimo na katika kutatua changamoto katika maeneo yao.

Kwa ujumla matendo ya kuthamini maadili ni muhimu katika maisha yetu ya kila siku. Hii husaidia kuishi salama katika jamii inayotuzunguka.

Zoezi la jumla

1. *Oanisha maneno kutoka sehemu* **A** *na sentensi zilizopo katika sehemu* **B** *kwa kuandika herufi ya jibu sahihi katika nafasi uliyopewa.*

Na	Sehemu A	Jibu	Sehemu B
i.	Kutii sheria		A. kuwapenda, kuwaheshimu na kuwasaidia watu wengine
ii.	Kujali		B. kuwahi shuleni
iii.	kujithamini		C. kufanya matendo ya pamoja
iv.	Kushirikiana		D. kujijali na kujali watu wengine

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 69 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Andika neno **NDIYO** mbele ya sentensi ambayo ni kweli na neno **HAPANA** mbele ya sentensi ambayo si kweli.
   i. Kuvuka barabara maeneo yenye alama za pundamilia huonesha utii wa sheria za usalama barabarani.
   ii. Kuwasalimia wenzetu na waliotuzidi umri ni matendo ya kuheshimu watu wengine.
   iii. Kufuata taratibu na kanuni za shule na nyumbani ni utii wa sheria.
   iv. Ushirikiano haujengi uhusiano.
3. Orodhesha mambo matatu (3) uliyojifunza kuhusu kujithamini.
4. Andika matendo matatu (3) ya kuonesha utii wa sheria shuleni.
5. Andika matendo matatu (3) ya kuonesha utii wa sheria nyumbani.
6. Andika matendo matatu (3) ya kuonesha utii wa sheria za barabarani.
7. Andika matendo mawili (2) ya kujali watu wengine.
8. Taja faida mbili (2) za kushirikiana na watu wengine.

Msamiati

Kejeli utani au sifa zisizo za kweli
Ufanisi hali ya kufanya kazi na kupata mafanikio
Ushindani hali ya kufanya kitu kwa kushindana

FOR ONLINE USE ONLY

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 70 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Sura ya Tano

Maarifa na ujuzi wa asili wa jamii

Utangulizi

Katika sura hii utajifunza kuhusu maarifa na ujuzi wa asili wa jamii inayokuzunguka na maadili yake. Pia, utajifunza kuhusu maarifa na ujuzi katika utunzaji wa mazingira, dawa na dini na maadili yake. Vilevile, utajifunza umuhimu wa maarifa na ujuzi wa asili kwa jamii. Umahiri utakaoupata katika sura hii utakuwezesha kutumia maarifa na ujuzi wa asili katika shughuli za uchumi, utunzaji wa mazingira, dawa za asili na dini katika jamii inayokuzunguka.



Fikiri

Maarifa na ujuzi wa asili katika jamii inayokuzunguka.

Dhana ya maarifa na ujuzi wa asili wa jamii

Maarifa na ujuzi wa asili wa jamii ni nini?

Kazi ya kufanya namba 1



Andika mambo unayoweza kuyatenda na eleza kwa nini unaweza kuyatenda.

Tumeweza kuyatenda mambo tuliyoyaandika kwa sababu ya maarifa au ujuzi tulionao.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 71 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Angalia picha katika Kielelezo namba 1, kisha fanya zoezi linalofuata.



Kielelezo Namba 1: *Ujuzi na maarifa katika kutenda*

Zoezi la 1

1. Ainisha shughuli wanazofanya katika Kielelezo namba 1.
2. Eleza ni kwa nini wanaweza kufanya shughuli wanazozifanya.

Watu huweza kutenda jambo fulani kutokana na maarifa na ujuzi walionao. Maarifa na ujuzi ni nini? Maarifa na ujuzi ni vitu viwili tofauti lakini vinavyohusiana na kutegemeana.

Maarifa hutupa ufahamu wa hali, habari, na maelezo yanayohusu namna ya kutenda jambo. Maarifa hayo yanaweza kuwa ya kijamii, kisayansi, kiutamaduni, au kiroho. Ujuzi hutupa uwezo wa kiufundi, kisanii au kijamii wa kutumia maarifa tuliyonayo katika kufanya kazi au kutenda. Ujuzi unaweza kuwa wa asili, yaani unaotokana na mazingira na teknolojia ya asili. Pia, unaweza kupatikana

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 72 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kutokana na teknolojia za kisasa kama vile za viwandani. Ukiwa na maarifa bila ujuzi huwezi kutenda au kufanya kazi kwa ufanisi. Katika sehemu hii tutajifunza kuhusu maarifa na ujuzi wa asili wa jamii zetu katika nyanja mbalimbali.

Maarifa na ujuzi wa asili katika uchumi

Jamii zetu zina maarifa na ujuzi wa asili katika shughuli za uchumi kama vile kilimo, uvuvi, ufinyanzi na uhunzi.

Maarifa na ujuzi wa asili katika Kilimo

Maarifa na ujuzi wa asili katika kilimo vilihusisha stadi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuchimba, kupanda na kukwatua majani. Pia, kilimo kilifanyika kwa kutengeneza matuta. Kilimo kilifanyika maeneo ya udongo wenye rutuba na mvua (chunguza Kielelezo namba 2). Samadi ilitumika kama mbolea ili kuongezea udongo rutuba.



Kielelezo namba 2: *Kilimo kwa kulima matuta*

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 73 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Pia, jamii za kale zilikuwa na maarifa na ujuzi katika kilimo cha umwagiliaji. Umwagiliaji ulifanyika kwa kutumia mito ya asili na maji yanayotiririka kutoka milimani. Mfano, maeneo ya Engaruka, Arusha kilimo cha umwagiliaji kilifanyika kwa kujenga mifereji kwa mawe kama matuta kutoka katika ukingo wa bonde la Ufa. Hii ilifanyika ili kuhifadhi na kupitisha maji kwa ajili ya umwagiliaji kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 3.



Kielelezo namba 3: *Mfereji uliojengwa kwa mawe kama matuta ili kukinga maji kwa ajili ya umwagiliaji*

Aidha, katika maeneo mengine maji ya mvua yalitengenezewa mabwawa yaliyowekewa kingo ili kutunza maji kwa muda mrefu hata baada ya msimu wa mvua kupita. Maarifa na ujuzi huu wa asili ulikuwepo hata kabla ya kuja kwa teknolojia za kilimo kutoka nchi za kigeni.

Jamii zililima mazao ya asili ya mizizi kama vile viazi vitamu, viazi vikuu na magimbi (chunguza mfano katika Kielelezo namba 4). Pia, walilima mazao kama vile mtama, uwele na ulezi. Haya ni baadhi tu ya mazao ya asili.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 74 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Viazi vya kuning'inia



Magimbi



Vianzi vitamu



Viazi vikuu

Kielelezo namba 4: *Baadhi ya mazao ya asili*

Zoezi la 2

1. Eleza maarifa na ujuzi mwingine wa asili katika kilimo katika maeneo yanayokuzunguka.

Maarifa na ujuzi wa asili katika uvuvi

Maarifa na ujuzi wa asili katika uvuvi vilifanyika kwa kutumia nyavu, ndoano, madema, mitumbwi na mitego ya asili ya kuvulia samaki kama vile matenga. Chunguza Kielelezo namba 5 na 6 kama mifano ya vyombo vilivyotumika katika uvuvi.



Kielelezo namba 5: *Maarifa na ujuzi wa asili wa jamii katika uvuvi*

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 75 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Nyavu ya kuvua samaki Ndoano za kutega samaki

Kielelezo namba 6: *Zana za asili za uvuvi*

Uvuvi ulifanyika maeneo yenye mito, maziwa, bahari, mabwawa na madimbwi ya maji mengi. Wavuvi walifunga ndoano kwa kamba na kuweka chambo ili kutega samaki. Nyavu pia zilitupwa kwenye maji kuvua samaki.

Maarifa na ujuzi wa asili katika ufugaji

Maarifa na ujuzi katika ufugaji vilifanyika kwa kufuga mifugo katika maeneo yenye nyasi ili kupata chakula cha mifugo. Mifugo iliyofugwa ni pamoja na ng'ombe, mbuzi na kondoo (chunguza Kielelezo namba 7).



Kielelezo namba 7: *Maarifa na ujuzi wa asili katika ufugaji*

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 76 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Pia, jamii zilikuwa na maarifa na ujuzi wa kufuga nyuki, sungura, kuku na bata. Ufugaji ulifanyika katika maeneo yenye nyasi na maji ya kutosha ili kuipatia mifugo malisho na maji. Mifugo ilifanyiwa usafi kwa kupitishwa kwenye maji ya mito na kutumia dawa za asili ili kuua wadudu. Vilevile, jamii zilikuwa na maarifa na ujuzi wa kutengeneza mafuta ya samli kwa kutumia maziwa yatokanayo na wanyama.

Maarifa na ujuzi wa asili katika uwindaji

Jamii zinazoishi maeneo ya misitu zilijihusisha na uwindaji. Maarifa na ujuzi wa asili katika uwindaji vilihusisha matumizi ya nyavu, mitego, mikuki, mishale na upinde. Pia, wanyama kama mbwa walitumika katika kuwinda (chunguza Kielelezo namba 8). Vilevile, dawa maalumu zilitumika kupunguza nguvu za wanyama wakubwa wakati wa uwindaji.



Kielelezo namba 8: *Maarifa na ujuzi katika uwindaji*

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 77 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Angalia mifano ya mitego iliyotumika katika shughuli za uwindaji katika Kielelezo namba 9.



Kielelezo namba 9: *Mitego ya asili ya kutegea wanyama na ndege*

Aidha, jamii zetu zilikuwa na maarifa na ujuzi wa asili katika ususi, ufinyanzi, upishi na uhunzi. Baadhi ya jamii hizi ziliweza kufua chuma na kutengeneza bidhaa za chuma kwa ustadi mkubwa. Mfano wa jamii hizi ni zile za maeneo ya Karagwe, Ufipa na Ugweno. Zana walizotengeneza zilitumika katika kilimo, ufugaji, uvuvi na uwindaji. Maarifa na ujuzi katika uhunzi vilichangia kukua kwa shughuli za uchumi katika jamii. Hivyo, jamii zilizalisha ziada.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 78 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kazi za kufanya namba 2



Fanya uchunguzi kuhusu shughuli za kilimo, uwindaji, ufugaji au uvuvi zilizopo kwa sasa na kisha fananisha na maarifa na ujuzi wa asili.

Historia ya maarifa na ujuzi wa asili katika jamii

Maarifa na ujuzi wa asili wa jamii vina historia yake. Maarifa na ujuzi wa asili viliendana na mazingira waliyoishi wanajamii husika. Shughuli za kilimo, ufugaji, uwindaji, uvuvi na uhunzi zilisababishwa na kuwepo kwa mazingira ya jamii husika. Kwa mfano, jamii zilizoishi maeneo yenye mvua za kutosha na udongo wenye rutuba zilijishughulisha na shughuli za kilimo. Jamii zilizoishi kando ya mito, maziwa na bahari zilifanya shughuli za uvuvi. Maarifa na ujuzi wa asili wa kufanya shughuli za uchumi vililirithishwa kutoka kizazi hadi kizazi. Wazee wenye stadi husika waliwafundisha vijana kwa vitendo. Pia, watu maalumu wenye maarifa na ujuzi, kama vile uhunzi, uchongaji na uwindaji walitumika katika kuwafundisha vijana. Hivyo, kila mwanajamii alikuwa na wajibu wa kufanya kazi na kushiriki katika shughuli za uchumi ili kuendeleza shughuli za kiuchumi katika jamii zao. Watu ambao hawakufanya kazi walikuwa ni wazee, watoto na wagonjwa. Makundi haya yaliruhusiwa kuwa tegemezi. Hii ilisaidia maarifa na ujuzi wa asili kurithiwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Jamii ya sasa inao wajibu wa kujifunza maarifa na ujuzi huu wa asili na kuviendeleza. Jamii zetu kwa sasa zinaweza kurithi maarifa na ujuzi wa asili kwa kushiriki shughuli za kijamii. Tunaposhiriki katika shughuli hizo tunapata nafasi ya kuona, kusikia na kuiga kwa kutenda. Pia, jamii ya sasa inaweza kujifunza maarifa na ujuzi huu shuleni na nyumbani.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 79 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Usomaji wa vitabu unaweza kutusaidia kupata maarifa na ujuzi wa asili uliopo katika jamii kwa sasa. Kujifunza mambo mbalimbali huongeza maarifa na ujuzi wetu. Vilevile, jamii kwa sasa inaweza kushiriki mafunzo, kufanya mazoezi na kufanya kazi pamoja na wenye maarifa na ujuzi huu wa asili ili kujifunza. Pia, jamii inaweza kuendeleza na kuboresha maarifa na ujuzi wa asili ili kuongeza ufanisi wa shughuli tunazozifanya. Ni muhimu kujifunza mambo mapya ili kuendelea kuongeza maarifa na ujuzi wetu katika maisha.

Zoezi la 3

1. Bainisha mbinu nyingine za kujifunza maarifa na ujuzi wa asili katika jamii unayoishi.

Maadili katika maarifa na ujuzi wa jamii katika uchumi

Je, unafikiri, jamii za kale zingeweza kurithi maarifa na ujuzi wa jamii zao kama wasingezingatia maadili? Utendaji wa maarifa na ujuzi wa jamii unahitaji kuzingatia maadili.

Kazi ya kufanya namba 3



Chunguza na andika maadili yaliyozingatiwa katika utendaji wa shughuli za uchumi katika eneo linalokuzunguka.

Jamii za kale zilizingatia maadili katika kudumisha maarifa na ujuzi wa asili katika shughuli za uchumi. Baadhi ya maadili yaliyozingatiwa ni:

(a) Kufanya kazi kwa bidii. Hii ilisaidia kufikia malengo yao;

(b) Kuwa mbunifu katika kufanya kazi. Hii ilisaidia teknolojia za asili kuendelea kukua na kuendana na wakati;

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 80 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c) Kudumisha uhusiano mzuri na watu waliofanya nao kazi. Hii ilisaidia kuongeza ufanisi wa kazi. Pia, waliweza kujifunza kutoka kwa watu wengine;
(d) Kuepuka vitendo viovu kama vile dhuluma na lugha za matusi. Hii ilisaidia kujenga uhusiano mwema;
(e) Kuwa makini katika kufanya kazi. Hii ilisaidia kuongeza ufanisi na kujifunza kwa ufasaha; na
(f) Kuepuka uvivu. Hii ilisaidia kuwa na bidii katika utendaji kazi.

Kazi ya kufanya namba 4



Orodhesha mambo uliyojifunza kuhusu maadili katika kudumisha maarifa na ujuzi wa asili wa jamii.

Maarifa na ujuzi wa asili katika utunzaji wa mazingira

Jamii za kale zilitumia zaidi mfumo wa imani za jadi zilizoambatana na miiko katika kujenga maadili ya kulinda na kutunza mazingira. Kwa mfano, miiko ya kimaadili ilitumika kulinda rasilimali adimu kama vile aina ya miti, wanyama na ndege. Kulikuwa na miiko ya kuzuia kufua, kuoga na kujisaidia haja kubwa au ndogo katika mabwawa, mito au maziwa yaliyotumika kwa matumizi ya maji ya nyumbani. Mabwawa mengine yalitengwa kama mahali "patakatifu." Haikuruhusiwa kuvua samaki au kuchafua bwawa "takatifu". Watu waliamini kuvunja maadili yale ni kuhatarisha mazingira.

Imani zilitumika kulinda mazingira. Misitu, milima, mapori, mapango, mabwawa na chemchemi zilitengwa kama maeneo ya "miungu." Maeneo haya yalitengwa kwa ajilli ya

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 81 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kufanyia ibada za asili. Hivyo, maeneo haya yaliheshimiwa na kulindwa na watu wote. Waliamini kuharibu maeneo haya kungesababisha kifo na majanga kama magonjwa kwenye familia na ukoo. Jamii za kale ziliamini kuwa miungu inaishi katika mazingira. Jamii iliamini kuwa uharibifu wa mazingira kama kukata miti ovyo, kuua wanyama ovyo na kuchafua vyanzo vya maji ni chukizo kwa miungu. Waliamini miungu ikikasirika jamii itapata laana na majanga kama ukame, njaa na magonjwa ya mlipuko. Pia, watu waliamini kwamba iwapo mtu ataenda kinyume na kuharibu mazingira, atakufa kwa kuvunja miiko.

Pia, jamii za kale zilikuwa na maarifa na ujuzi wa kutumia mazingira yao kutambua majira ya mwaka na muda. Hapo kale, hapakuwa na saa wala kalenda kama sasa. Watu walikuwa na maarifa na ujuzi wa kutambua majira ya mwaka na saa kwa kutumia maarifa na ujuzi wa mazingira. Jamii zilitumia maarifa na ujuzi wa asili wa mazingira kutambua majira ya mvua na wakati wa kulima, kupanda na kuvuna mazao. Vilevile, mazingira yalitumika kutambua mazao yanayofaa kulimwa katika maeneo wanayoishi na wakati wa kuyalima. Maarifa na ujuzi katika utunzaji wa mazingira vilisaidia jamii kupunguza majanga yanayosababishwa na ukame.

Zoezi la 4

1. Andika mambo uliyojifunza kuhusu maadili ya utunzaji wa mazingira.
2. Andika umuhimu wa maadili uliyojifunza kwa utunzaji wa mazingira ya sasa.

Jamii za kale zilitambua wajibu wa kulinda misitu, miamba, milima, mito, maziwa, wanyama, ndege na kadhalika. Jamii

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 82 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ilitambua kuwa mahitaji yao yalitokana na rasilimali asili katika mazingira yao. Jamii ilitambua wajibu wa kutunza mazingira kwa faida yao na vizazi vijavyo. Mazingira yaliwapatia mvua, chakula na malighafi za kutengezea dawa; kwa mfano, mizizi, majani na magome ya miti, pamoja na malighafi za ujenzi wa nyumba.

Kazi ya kufanya namba 5



Bainisha mambo uliyojifunza kuhusu utunzaji wa mazingira katika jamii za kale.

Maarifa na ujuzi wa mazingira ni muhimu kwa maendeleo ya jamii. Maarifa na ujuzi wa mazingira katika jamii za kale vilisaidia:

(a) Kumudu mazingira ya jamii kama vile kutambua majira ya mwaka na wakati;

(b) Kutabiri majanga kwa kutumia maarifa na ujuzi wa historia; na

(c) Kuepuka hatari na majanga yanayotokana na uharibifu wa mazingira kama magonjwa, ukame, joto na kadhalika.

Hivyo, ni jukumu letu kuwa na maarifa na ujuzi wa kutunza mazingira yetu. Hii itatusaidia kupata mvua za kutosha, kupata hewa safi na kuepuka magonjwa ya mlipuko na ukame.

Maarifa na ujuzi wa asili katika dawa

Jamii za kale zilikuwa na ujuzi na maarifa katika dawa. Maarifa na ujuzi vilikuwa muhimu kwa ajili ya kulinda na kutunza afya ya jamii.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 83 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kazi ya kufanya namba 6

Waulize wazazi au walezi kuhusu dawa tunazotumia wakati tunapopata magonjwa na orodhesha dawa hizo.

Idadi kubwa ya watu katika jamii hutumia dawa ili kulinda na kurudisha afya njema. Kama ilivyo kwa jamii za sasa, jamii za kale zilitumia dawa kutibu magonjwa mbalimbali, ingawa kuna tofauti kati ya dawa zinazotumika sasa na zile zilizotumika katika jamii za kale katika kulinda afya na kutibu magonjwa. Tofauti hizi zipo katika maarifa na ujuzi uliopo katika utengenezaji na matumizi ya dawa husika. Utengenezaji wa dawa za kisasa hutegemea maarifa na ujuzi wa viwanda. Angalia mfano wa dawa za kisasa katika Kielelezo namba 10.



Kielelezo namba 10: *Dawa za Kisasa*

Utayarishaji wa dawa za asili ulihusisha maarifa na ujuzi wa asili. Vitu asilia kama vile miti, majani, magome ya miti, mizizi na maua vilitumika kutengeneza dawa za asili.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 84 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Angalia mfano wa vitu vilivyotumika kutengenezea dawa za asili katika Kielelezo namba 11.



Kielelezo namba 11: *Majani, mizizi na magome ya kutengenezea dawa za asili*

Maarifa na ujuzi wa asili katika utayarishaji wa dawa za asili ulifanyika kwa kuchemsha, ambapo dawa ama zilichanganywa na maji au supu. Pia, dawa hizi zilitengenezwa kwa kupondwa, kutwangwa au kusagwa. Dawa za asili zilitumika kwa kunywa, kupaka, kufukiza, kuoga, kuchua, kujikanda au kunusa. Dawa za asili zilitumika katika kutibu na kuzuia magonjwa.

Baadhi ya dawa zilizopo hospitali zimetokana na dawa za asili. Tofauti ni teknolojia ya kuzitengenezea na namna ya kuzihifadhi dawa za kisasa.

Kazi ya kufanya namba 7

Fanya uchunguzi katika maeneo unayoishi kuhusu maarifa na ujuzi wa kutayarisha na kutumia dawa za asili.

Ni wazi kuwa maarifa na ujuzi wa dawa za asili ukiendelezwa vitakuwa suluhisho la tiba katika jamii yetu ya sasa. Dawa hizi za asili zimezisaidia jamii zetu, hasa katika kipindi cha mlipuko wa ugonjwa wa uviko 19. Dawa hizi zinatibu kwa kiwango cha dawa za kisasa zinazotolewa katika hospitali zetu. Chunguza matumizi ya dawa za asili zinavyotumika kutibu katika Kieleleza namba 12.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 85 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Kielelezo namba 12: *Matumizi ya tiba za asili kwa kujifukiza na kunywa*

Maadili katika maarifa na ujuzi wa asili katika dawa

Maarifa na ujuzi wa asili katika dawa huzingatia maadili. Maadili yalizingatiwa katika utayarishaji na matumizi ya dawa ili kujenga afya ya jamii. Maadili yaliyozingatiwa katika utayarishaji wa dawa ni pamoja na:

(a) Kuzingatia usafi wa vyombo na mahali pa kutayarishia dawa;

(b) Kutumia kanuni sahihi za utayarishaji kulingana na aina ya dawa; na

(c) Kuzingatia ukweli na uaminifu katika utayarishaji, usambazaji na matumizi ya dawa.

Pia, maadili yalisisitizwa katika matumizi ya dawa ili kuongeza ufanisi wa dawa. Maadili hayo ni pamoja na:

(a) Kuzingatia kanuni za matumizi ya dawa ama kupaka, kufukiza, kuoga au kunusa. Kukiuka maadili katika matumizi ya dawa huleta madhara;

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 86 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Kusisitiza matumizi ya dawa kwa wakati uliopangwa, kabla au baada ya chakula au pamoja na chakula;
(c) Kutumia dawa kwa kiasi kilichopangwa; na
(d) Kufanya mazoezi mbalimbali ya mwili wakati wa matibabu.

Jamii zilikuwa na watu maalumu wenye maarifa na ujuzi wa asili wa kutengeneza dawa. Watu hawa ndio waliotoa maelekezo ya matumizi ya dawa kwa wagojwa. Hadi sasa baadhi ya jamii zimeendelea kurithi maarifa na ujuzi wa asili katika dawa.

Kazi ya kufanya namba 8



Fanya uchunguzi kuhusu umuhimu wa maarifa na ujuzi wa tiba za asili kwa jamii ya sasa.

Maarifa na ujuzi wa dawa za asili una nafasi katika tiba ya jamii kwa sasa. Hivyo, jamii ya sasa inapaswa kuzienzi tiba za asili na kutafuta jinsi ya kuzitumia kama tiba mbadala ili kuimarisha afya ya Watanzania.

Zoezi la 5

1. Taja mambo ya kujifunza kutokana na maarifa na ujuzi wa asili wa jamii katika dawa.
2. Eleza wajibu wa jamii katika kuendeleza maarifa na ujuzi wa asili katika dawa kwa sasa.

Maarifa na ujuzi wa jamii katika dini

Jamii za Kitanzania zilikuwa na dini za asili. Dini ilikuwa ni sehemu ya asili za jamii za Watanzania. Chunguza Kielelezo namba 13 kuhusu maadili katika dini za asili.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 87 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Kielelezo namba 13: *Watu wakifanya ibada nje ya pango*

Jamii zetu tangu kale ziliamini kuwapo kwa miungu yenye uwezo wa kutatua changamoto mbalimbali. Hivyo, jamii ziliabudu miungu katika maeneo mbalimbali kama vile katika makaburi, mapango, milima, chini ya majabali au miti mikubwa. Matambiko na sherehe zilizoendana na mila na desturi katika ibada zilifanyika wakati wa ibada za dini za asili. Dini ilitumika kutatua changamoto katika jamii kama vile uzazi, magonjwa na majanga kama ukame. Jamii ilikuwa na watu maalumu walioaminika kutengeneza mvua wakati wa ukame. Pia, jamii zilikuwa na kiongozi maalumu ambaye alisimamia dini za asili. Dini hizi zilithaminiwa, ziliheshimiwa na zilirithishwa kutoka kizazi hadi kizazi katika jamii husika. Jamii iliamini kuwa kuheshimu na kuthamini dini ni chanzo cha baraka kwa jamii kama vile kuongezeka kwa mvua, mazao na uzazi. Pia, waliamini ukiukaji wa miiko katika dini ni chanzo cha laana, magonjwa na majanga katika jamii.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 88 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Maadili katika dini

Maadili katika dini yalizingatiwa katika kuabudu na kusali katika maisha ya kila siku. Kwa mfano watu walisali kwa:

(a) Kufunga macho wakati wa kusali;
(b) Kupiga magoti;
(c) Kuweka mikono juu; na
(d) Kuinama wakati wa kusali.

Zoezi la 6

1. Eleza umuhimu wa maarifa na ujuzi wa asili katika dini kwa jamii ya sasa.

Maarifa na ujuzi wa asili ni muhimu kwetu kwani husaidia kuthamini taaluma na teknolojia za jadi katika ufanisi wa kazi na mazingira. Pia, ni muhimu katika kujenga afya na kulinda rasilimali.

Zoezi la jumla

Jibu maswali yafuatayo:

1. Taja mambo manne (4) uliyojifunza kuhusu maarifa na ujuzi wa asili.
2. Andika tofauti mbili (2) kati ya maarifa na ujuzi wa asili na wa sasa katika kilimo.
3. Orodhesha mbinu mbili (2) zilizotumika katika kujifunza maarifa na ujuzi wa asili.
4. Eleza wajibu wa jamii ya sasa katika kuendeleza maarifa na ujuzi wa asili.
5. Andika mambo manne (4) uliyojifunza kuhusu maarifa na ujuzi wa asili katika utunzaji wa mazingira.
6. Eleza tofauti mbili (2) zilizopo kati ya maarifa na ujuzi wa dawa za asili na za sasa.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 89 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

7. Andika neno **NDIYO** mbele ya sentensi ambayo ni kweli na neno **HAPANA** mbele ya sentensi ambayo si kweli.
   (i) Matumizi ya ndoano na nyavu ni maarifa na ujuzi wa asili katika uvuvi.
   (ii) Dini ni sehemu ya maarifa na ujuzi wa asili kwa jamii za Kitanzania.
   (iii) Viazi vikuu, magimbi, viazi mviringo, mahindi na ulezi ni mazao ya asili.
   (iv) Kilimo cha umwagiliaji na matuta ni maarifa na ujuzi wa asili katika kilimo.
   (v) Matumizi ya mikuki, mishale na upinde ni maarifa na ujuzi wa asili katika uwindaji.

Msamiati

Afya	hali ya uzima, kuwa na siha
Asili	chimbuko au chanzo cha sababu ya uwepo wa kitu au jambo
Chambo	chakula kinachotumika kutega samaki
Dawa	majimaji, vidonge, unga au mafuta ambayo hutumika kwa lengo la kutibu au kuponya ugonjwa
Dini	imani inayohusisha kuwapo kwa Mungu au miungu
Kuchua	kusugua juu ya ngozi kwa kutumia mikono yenye dawa kwa ajili ya kuondoa maumivu
Kufukiza	kumfanyia mgonjwa dawa kwa kumgubika kwenye mvuke

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 90 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kuoga	kumwagia kitu mwilini, mfano maji au dawa, kwa lengo la kusafisha au kuondoa uchafu
Kupaka	kusugua taratibu kitu kama mafuta au unga juu ya kitu kingine
Kusaga	tendo la kupondaponda kwa kutumia jiwe
Mila	taratibu za kimaisha za mwenendo wa kufanya mambo zinazofuatwa na jamii fulani kulingana na historia na utamaduni wao
Ndoano	kipande cha waya kilichopinda upande mmoja na hufungwa kamba upande mwingine, hutumika kuvulia samaki
Nusa	tambua harufu kwa kutumia pua
Nyavu	kifaa chenye matundu kilichosukwa kwa nyuzi ambacho hutumika katika uvuvi
Samadi	mbolea inayotokana na kinyesi cha wanyama kama mbuzi, ng'ombe, kondoo au kuku
Tiba	kitu au dawa ya kuponya magonjwa
Twanga	pigapiga ndani ya kinu kwa kutumia mchi kwa lengo la kutoa maganda, kupata unga au kulainisha
Ufinyanzi	tendo la kutengeneza maumbo au vitu kwa kutumia udongo na mikono
Ususi	kitendo cha kupitisha chane za ukindu kwa mtindo maalumu wakati wa kutengeneza ukili

FOR ONLINE USE ONLY

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 91 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Sura ya Sita

Asili za jamii za Watanzania

Utangulizi

Katika sura iliyopita ulijifunza kuhusu maarifa na ujuzi wa asili katika shughuli za uchumi, utunzaji wa mazingira, dini na dawa. Katika sura hii utajifunza asili za jamii za Watanzania katika utamaduni, mavazi, chakula, ngoma, nyimbo na michezo. Pia, utajifunza kuhusu maadili ya asili ya jamii hizi. Umahiri utakaoupata utakuwezesha kuthamini asili za jamii za Watanzania na maadili yake.



Fikiri

Fikiri kuhusu asili za jamii za Watanzania.

Asili za jamii

Tunapoeleza kuhusu asili za jamii tunalenga chanzo cha mfumo mzima wa jamii husika. Jamii za Watanzania zina makabila yenye asili tofauti. Asili za makabila yaliyopo nchini zimesababisha kuwepo kwa tofauti za tamaduni, ngoma, nyimbo, michezo, mavazi na vyakula. Aidha, pamoja na tofauti hizo, jamii hizi zina mfanano wa karibu kitabia, kimaadili, kiimani, pamoja na lugha. Hii inatokana na ukweli kuwa jamii nyingi za Watanzania kiasili zimetoka katika chimbuko linaloshabihiana katika makundi ya asili zao. Mfanano huo, kwa upande mwingine, umesababishwa na mwingiliano wa makabila kutokana na shughuli mbalimbali za uchumi na

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 92 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kijamii. Mwingiliano kati ya kabila na kabila husababisha jamii kujifunza na hata kuiga maadili ya jamii zingine.

Kazi ya kufanya namba 1



Waulize wazazi au walezi, kisha andika mambo yanayosisitizwa katika kabila lako.

Kuna tofauti ya tabia, mavazi, chakula na lugha kati ya jamii moja na nyingine. Tofauti hizi ndizo zinazotofautisha na kutambulisha jamii za Watanzania. Pamoja na tofauti zilizopo kati ya kabila na kabila, kuna mfanano wa mambo fulani. Mfanano uliopo unatokana na kuwepo kwa misingi ya kimaadili iliyojengwa kwa kanuni na taratibu zilizokubalika katika jamii za Watanzania kama misingi ya maadili. Misingi hii kwa maana nyingine ndiyo inayounda utamaduni wa Mtanzania.

Utamaduni

Kama ilivyo shuleni na nyumbani, jamii zetu zimeweka taratibu, miongozo, kanuni na sheria zinazowawezesha watu wake kuishi kwa kutenda au kufikiri katika mazingira yao. Taratibu, kanuni na sheria zilizopo katika jamii, kwa ujumla wake, zinajulikana kama utamaduni. Pia, utamaduni ni mwongozo wa namna ya kuishi, kufikiri na kutenda. Mwongozo huu una sheria, kanuni na taratibu zilizokubalika katika jamii husika. Watu hutambuliwa na hutofautishwa kwa kigezo cha tamaduni zao.

Kazi ya kufanya namba 2



Waulize wazazi au walezi kuhusu utamaduni wa kabila lako na tofauti zilizopo kati ya tamaduni hizo na za sasa.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 93 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Jamii zina tamaduni zenye taratibu, sheria na kanuni tofauti zinaoongoza katika kutenda na kufikiri. Taratibu, sheria na kanuni hizi ndizo huunda mila na desturi za jamii. Ni mila kwa sababu zinaonesha taratibu za kimaisha za mwenendo na jinsi ya kufanya mambo. Taratibu hizi hufuatwa na jamii fulani kulingana na historia na utamaduni wao. Pia ni desturi kwa sababu huonesha mienendo, taratibu au kanuni za jamii zinazotendwa mara kwa mara. Mila na desturi hizi huwa ni kielelezo cha jamii fulani kwani hutofautiana kati ya jamii na jamii. Kimsingi, utamaduni ni urithi muhimu wa jamii husika katika kujenga na kudumisha uzalendo.

Kiasili, jamii za Kitanzania zilikuwa na misingi ya kimaadili yenye tamaduni zinazofanana. Mfanano katika misingi ya utamaduni ndio unaojenga utamaduni wa Mtanzania.

Kuheshimiana

Misingi ya kitamaduni katika asili za jamii za Kitanzania imejengwa katika misingi ya kuheshimiana na upendo. Misingi hii katika jamii huoneshwa katika vitendo vya kimaadili katika kusalimiana, kusaidiana na kujali watu wengine. Aidha, pamoja na kuwepo kwa matendo tofauti katika kusalimiana, kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 1, kiasili jamii zilithamini matendo ya kuheshimiana, kuheshimu na kujali watu wengine, wakubwa kwa wadogo.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 94 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Chunguza matendo ya kusalimiana katika Kielelezo namba 1, kisha jibu zoezi linalofuata.



Kielelezo namba 1: *Matendo ya kusalimiana*

Zoezi la 1

1. Watu waliooneshwa katika Kielelezo namba 1 wanasalimiana kwa namna gani?
2. Taja namna mbili (2) nyingine za kusalimiana ambazo hazikuoneshwa kwenye Kielelezo namba 1.
3. Je, katika jamii yako watu wa rika mbalimbali wanasalimianaje?

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 95 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kazi ya kufanya namba 3

Andaa na onesha onyesho la matendo ya kusalimiana katika jamii za Watanzania.

Watu hufanya matendo tofauti katika kusalimiana katika jamii kulingana na tamaduni zao. Matendo haya katika kusalimiana yamejengwa katika misingi ya utu, upendo na heshima kwa watu wengine.

Kushirikiana

Misingi ya tamaduni za jamii za Watanzania ilisisitiza ushirikiano na watu wengine. Ushirikiano ulisisitizwa katika jamii ili kuongeza ufanisi katika utendaji wa shughuli mbalimbali katika jamii. Miiko, misemo na methali kama *kidole kimoja hakivunji chawa* ilitumika kusisitiza ushirikiano katika jamii zetu (chunguza Kielelezo namba 2). Jamii zilishirikiana katika mambo ya kiuchumi na kijamii, bila kujali hali ya mtu. Utu na upendo vilizingatiwa ili kukuza nguvu ya kushirikiana na kuhusiana katika jamii.



Kielelezo namba 2: *Watoto wakishirikiana kutengeneza maumbo*

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 96 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kupenda na kuthamini kazi

Misingi ya tamaduni za kijamii ilisisitiza kupenda na kuthamini kazi. Watu walithaminiwa kwa kupenda na kufanya kazi. Jamii zote za Watanzania zilisisitiza kufanya kazi. Kufanya kazi kulionesha uwajibikaji kwa mtu binafsi na jamii kwa ujumla.

Tabia njema

Tamaduni za jamii zilisisitiza tabia njema na kukemea tabia mbaya. Kila mtu alipaswa kutenda matendo yanayokubalika katika jamii. Adhabu zilitolewa bila kujali cheo wala umri. Hii ilisaidia kujenga uadilifu katika jamii za kale. Tabia njema zilihimizwa ili kujenga tabia ya watu kupendana, kusaidiana na kushikamana.

Kazi ya kufanya namba 4



Fanya uchunguzi mdogo na andika kuhusu misingi mingine ya utamaduni inayosisitizwa katika jamii inayokuzunguka.

Misingi iliyopo katika jamii za Kitanzania ilikuwa na umuhimu wa kuweka taratibu za maisha katika jamii. Taratibu hizo zililenga kujenga mshikamano bila kujali tofauti za jamii katika dini, elimu, imani wala rangi. Kwa ujumla, misingi ya utamaduni pamoja na mambo mengine ililenga katika:

(a) Kuhimiza jamii kufanya na kuthamini kazi;
(b) Kuhimiza usawa katika mgawanyo wa rasilimali na umiliki wake;
(c) Kuhimiza tabia ya kuheshimu na kujali utu wa mtu mwingine;

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 97 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(d) Kuhimiza malezi bora katika jamii;
(e) Kuthamini taaluma na teknolojia za jadi katika kujenga afya, ufanisi katika kazi na utunzaji wa mazingira na rasilimali;
(f) Kulinda na kuimarisha maadili katika jamii;
(g) Kujengea jamii uwezo wa kujiendeleza kimaisha kwa kuzingatia taratibu na kanuni za jamii zao;
(h) Kujenga tabia ya ushirikiano, mshikamano na moyo wa kusaidiana katika jamii; na
(i) Kujenga undugu na upendo katika jamii.

Ni muhimu kwa jamii zetu, kwa sasa, kudumisha asili za jamii za Watanzania katika tamaduni zetu na misingi yake ili kujenga uzalendo. Tunaweza kukuza maadili kwa sasa kwa kufanya matendo ya maadili yaliyosisitizwa na jamii zetu.

Kazi ya kufanya namba 5



Andika wajibu wako na wa jamii kwa sasa katika kudumisha utamaduni

Mavazi

Jamii za Kitanzania zilikuwa na mavazi ya asili yenye kutambulisha na kutofautisha jamii moja na nyingine.

Kazi ya kufanya namba 6



Waulize wazazi au walezi kuhusu aina, muundo na mwonekano wa mavazi ya kabila lako na tofauti ya mavazi ya asili na ya sasa.

Jamii zilikuwa na mavazi ya asili tofauti na mavazi tunayovaa sasa. Mavazi ya asili hutambulisha na kutofautisha jamii

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 98 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

moja na nyingine. Pamoja na tofauti hizo, kulikuwa na mambo yanayofanana katika mavazi yao. Kielelezo namba 3 kinaonesha baadhi ya mavazi ya makabila mbalimbali ya Kitanzania.



Mavazi ya kike ya Wadatoga



Mavazi ya kike ya Waha



Mavazi ya kike ya Wamasai



Vazi la kike la Wagogo



Vazi la kiume la Wamasai



Vazi la kiume la Wasukuma



Mavazi ya kiume ya Wangoni

Kielelezo namba 3: *Baadhi ya Mavazi ya jamii za Watanzania*

Mavazi ya asili ya Kitanzania yanasisitiza sifa zifuatazo:

(a) Mavazi ya heshima yenye kusitiri mwili, yaani mavazi yasiyoonesha maungo;

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 99 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Mavazi yanayoendana na mazingira na utamaduni wa jamii inayohusika;

(c) Mavazi nadhifu na yenye kupendeza; na

(d) Mavazi yanayoendana na shughuli inayohusika, kama vile sherehe, misiba na vita.

Kazi ya kufanya namba 7



Chunguza picha katika Kielelezo namba 3 na andaa onesho la mavazi ya asili ya aina mbalimbali.

Tunao wajibu hivi sasa kama watoto wa kuendeleza mavazi ya asili. Hivyo, ni vema kuepuka kuvaa mavazi yanayoonesha maungo ya mwili. Tunapaswa kuvaa mavazi ya heshima na yenye kusitiri mwili. Uvaaji wa nguo zenye kuonesha maungo ya mwili ni kinyume na maadili ya Kitanzania. Kuvaa mavazi ya heshima kunajenga heshima kwa mtoto na jamii inayomzunguka.

Kazi ya kufanya namba 8



Jadili na kueleza mambo uliyojifunza kuhusu mavazi ya asili ya jamii za Kitanzania na namna ya kuendeleza mavazi hayo kwa sasa.

Ngoma za asili

Ngoma za asili ni utamaduni wa Mtanzania. Jamii zilicheza ngoma kwa mitindo tofauti kama kuruka, kutingisha viungo vya mwili, kuchezesha miguu, kuchezesha mabega na kadhalika, kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 4.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 100 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Kielezo namba 4. *Mitindo ya kucheza ngoma za asili za Kitanzania*

Jamii za Kitanzania zilitumia ala kama vile ngoma, filimbi na marimba katika kucheza ngoma hizi za asili (chunguza Kielelezo namba 5).



Ngoma



Marimba ya mbao na vigongeo



Filimbi



Manyanga

Kielelezo namba 5: Baadhi ya ala za ngoma za asili za Kitanzania

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 101 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kazi ya kufanya namba 9

Chunguza ngoma ya asili za kabila mojawapo la Tanzania na fanya onyesho la ngoma hiyo.

Chunguza picha A, B na C katika Kielelezo namba 6, kisha fanya zoezi linalofuata.

A.



B.



C.



Kielelezo namba 6: *Matendo katika ngoma za asili*

Zoezi la 2

1. Eleza matendo yanayofanyika katika Picha A na B.
2. Eleza mitindo ya kucheza ngoma inayoonekana katika Picha C.

Nyimbo

Ngoma za asili ziliambatana na kuimba nyimbo. Nyimbo ziliimbwa kuendana na tukio. Baadhi ya nyimbo ziliimbwa kwa ajili ya kuonya na kufundisha jamii. Ala mbalimbali kama vile zeze, ngoma na filimbi zilitumika wakati wa kuimba. Angalia mfano katika Kielelezo namba 7.



Kielelezo namba 7:
Ala ya mziki ijulikanayo kama zeze

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 102 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Nyimbo zilitumika kama sehemu ya burudani katika jamii. Kulikuwa na nyimbo zilizoimbwa kwa matukio mbalimbali, mfano wakati wa mavuno, sherehe za jando na unyago, harusi na misiba. Nyimbo hizi ziliimbwa kwa ajili ya kufundishia, kuonya na kuburudisha jamii.

Kazi ya kufanya namba 10



Jadili tofauti zilizopo kati ya nyimbo za kizazi kipya na nyimbo za asili katika kujenga maadili ya jamii kwa sasa.

Jamii ya sasa ina baadhi ya nyimbo zenye maudhui yanayoharibu maadili ya jamii. Ni wajibu kwa watoto kuepuka kuimba na kuiga matendo yasiyofaa yanayoambatana na baadhi ya nyimbo za muziki wa kizazi kipya. Hii itasaidia kujenga maadili yanayofaa katika jamii zetu kwa sasa.

Vyakula

Jamii za Kitanzania zilikuwa na vyakula mbalimbali vya asili.

Kazi ya kufanya namba 11



Waulize wazazi au walezi na andika kuhusu vyakula vya asili vya kabila lako.

Jamii zina asili ya vyakula vinavyofanana, ingawa kuna tofauti ya mapishi. Kwa mfano, jamii nyingi zilikuwa na chakula cha ndizi, ingawa mapishi ya ndizi yalitofautiana kati ya jamii na jamii. Mapishi ya ndizi ya asili hufanyika ama kwa kuchanganywa na nyama, maharagwe, samaki, njugu mawe, choroko au mbogamboga. Pia, ndizi huchomwa au huchanganywa na maharagwe, supu au maziwa na kukorogwa

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 103 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ili kupata chakula laini. Kielelezo namba 8 kinaonesha baadhi ya vyakula vya asili vya jamii za Kitanzania.



A. Ugali wa mtama



B. Ndizi za kuchoma



C. Ndizi zilizokorogwa



D. Kande



E. Viazi vitamu vilivyochemshwa

Kielelezo namba 8: *Baadhi ya vyakula vya asili vya jamii za Kitanzania*

Vyakula vya asili vilipikwa kwa kuchemshwa, kubanikwa, kuchomwa au kutumia mafuta ya asili kama vile nazi, karanga, kweme, samli na mawese. Vyakula vya asili vilisaidia jamii kupata nguvu, kujenga mwili, na kulinda miili dhidi ya maradhi. Watu waliishi kwa muda mrefu kutokana na kuwa na nguvu na afya ya mwili. Vyakula vya asili ya Kitanzania vina aina zote za virutubisho, yaani protini, wanga, vitamini, madini na mafuta.

Kazi ya kufanya namba 12

Andika tofauti kati ya vyakula vya asili vya jamii yako na vya sasa.

Mwingiliano wa makabila na kuingia kwa wageni katika jamii zetu kumeleta mabadiliko katika vyakula vyetu. Pamoja na

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 104 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mabadiliko hayo, jamii zetu zinapaswa kuthamini vyakula vyetu vya asili. Kula vyakula vya asili husaidia kudumisha utamaduni wetu. Pia, ni kiashiria cha kuwa wazalendo.

Michezo

Jamii zetu pia zina michezo ya asili. Baadhi ya michezo ilihitaji kutumia nguvu. Michezo hiyo ni mieleka, kuvuta kamba, masumbwi, kuruka kamba, mbio, rede na bao. Michezo hii ilichezwa ili kufanya mazoezi na kudumisha uhusiano na urafiki. Kielelezo namba 9 kinaonesha baadhi ya michezo ya asili.



A. Kuruka kamba



B. Kucheza bao



C. Mdako.



D. Rede

Kielelezo namba 9: *Michezo mbalimali ya asili*

Kazi ya kufanya namba 13

Fanya uchunguzi kuhusu michezo ya asili iliyopo katika maeneo unayoishi, kisha andika namna ya kuiendeleza.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 105 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Pia, jamii za Kitanzania zilikuwa na asili katika dini. Dini zilitumika katika kujenga maadili ya jamii. Vilevile, michoro na uchongaji wa vitu kama vinyago ilikuwa ni sehemu ya kuelezea asili za jamii za Watanzania.

Asili za jamii si jambo linalokuwa kwa muda mfupi. Hujengwa na watu kwa kipindi kirefu. Hivyo, tuna wajibu wa kudumisha asili za jamii za Watanzania kwa sasa.

Zoezi la jumla

Jibu maswali yafuatayo:

1. Andika mambo manne (4) uliyojifunza kuhusu asili za jamii katika utamaduni.
2. Eleza tofauti mbili (2) kati ya maarifa na ujuzi wa asili katika mavazi ya asili na ya sasa.
3. Eleza namna ya kuendeleza asili katika tamaduni kwa sasa.
4. Eleza tofauti mbili (2) kati ya vyakula vya asili na vya sasa.
5. Eleza umuhimu wa kutumia vyakula vya asili kwa sasa.
6. Eleza maadili yaliyozingatiwa katika mavazi ya asili.
7. Taja ala zilizotumika katika kucheza ngoma za asili.

Msamiati

Afya hali ya uzima, kuwa na siha
Banikwa kupika kwa joto
Chemshwa kupika kwa kuweka maji
Choma tendo la kuunguza kwa moto
Desturi mienendo, taratibu au kanuni za jamii zinazotendwa mara kwa mara
Dini imani inayohusisha kuwapo kwa Mungu au miungu

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 106 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Filimbi ala inayotoa sauti kwa kupulizwa

Hadithi masimulizi ya mambo yaliyotokea au ya kubuni

Kande chakula cha asili chenye mchanganyiko wa mahindi na maharagwe

Mafumbo maneno yenye kubeba maana zilizofichika

Manyanga ala ya muziki inayotengenezwa kwa kopo au kibuyu kilichotiwa mbegu kavu au kokoto

Mdako mchezo wa asili unaochezwa kwa kuchambua mawe yote yaliyo kwenye shimo bila kudondosha

Methali Usemi wenye mafundisho yaliyofichika

Mila taratibu za kimaisha za mwenendo wa kufanya mambo zinazofuatwa na jamii fulani kulingana na historia na utamaduni wao

Misemo vifungu vya maneno vyenye kubeba maana ya kimaadili

Miiko mambo yanayopigwa marufuku katika jamii fulani kwa mujibu wa imani, utamaduni na desturi zao

Onya tendo la kuelekeza mtu asitende jambo fulani kwa kumfafanulia athari za jambo hilo

Rede mchezo wa asili unaochezwa kwa kurushiana mpira kwa kumlenga wa katikati. Mlengwa hukwepa kupigwa au huvizia kudaka mpira, kisha kumpiga nao mmoja wapo kati ya waliourusha mpira

Uzalendo hali ya kupenda nchi au jamii kwa kuweka maslahi yake kwanza zaidi ya maslahi yako binafsi

Vitendawili semi za mafumbo ambazo humaanisha kitu fulani

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 107 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Sura ya Saba

Urithi na asili za jamii kwa maendeleo ya sasa

Utangulizi

Katika sura hii utajifunza kuhusu umuhimu wa urithi na asili za jamii na urithi wa kihistoria kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Pia, utajifunza mbinu za kutumia maarifa na ujuzi wa asili katika kuboresha ustawi wa jamii kwa sasa. Vilevile, utajifunza jinsi ya kusimulia maarifa na ujuzi wa asili, asili za jamii na urithi wa kihistoria katika mazingira ya nyumbani na shuleni. Mwisho, utajifunza thamani ya asili na urithi wa kihistoria katika jamii inayokuzunguka. Umahiri utakaoupata katika sura hii utakuwezesha kutumia urithi na asili za jamii kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa sasa.



Fikiri

Urithi na asili za jamii kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii

Umuhimu wa maarifa na ujuzi wa asili na urithi wa kihistoria

Kazi ya kufanya namba 1



Waulize wazazi au walezi umuhimu wa maarifa na ujuzi wa asili na urithi wa kihistoria uliopo katika maeneo yako katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Maarifa na ujuzi wa asili na urithi wa kihistoria una umuhimu katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa sasa.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 108 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kiuchumi

Urithi wa kihistoria ni muhimu kwa jamii katika uchumi kwa sababu Taifa hufaidika kwa kupata fedha za kigeni zinazolipwa na watalii nchini ambao huja kutembelea maeneo yenye urithi huo. Fedha zinazolipwa na wageni huchangia pato la taifa ambalo hutumika kuboresha miundombinu na huduma za jamii ili kuleta maendeleo nchini.

Maarifa na ujuzi wa asili katika shughuli za kilimo, ufugaji, uvuvi na uwindaji ni muhimu kwa maendeleo ya uchumi na jamii. Shughuli hizi ni chanzo cha:

(a) *Kipato kwa jamii na taifa;*
(b) *Kupata chakula na malighafi nyingine kwa ajili ya maendeleo ya uchumi nchini; na*
(c) *Kupata maarifa na ujuzi wa kuboresha shughuli za uchumi wa sasa.*

Kijamii

Maarifa na ujuzi wa asili na urithi wa kihistoria ni muhimu kwa maendeleo ya jamii. Hii ni kwa sababu:

(a) *Jamii hunufaika kutokana na fedha zinazolipwa na wageni kama gharama za malazi, chakula na vitu mbalimbali wanapokuja kutembelea maeneo yenye urithi wa kihistoria;*
(b) *Urithi wa kihistoria hutoa fursa mbalimbali za ajira kama vile biashara kwa wanajamii wanaozunguka eneo husika;*
(c) *Ujio wa wageni katika maeneo ya urithi wa kihistoria huitangaza nchi yetu katika uso wa dunia;*
(d) *Maarifa na ujuzi wa asili katika utunzaji wa mazingira ni muhimu kwa ajili ya kujifunza namna ya kutunza mazingira ya sasa;*
(e) *Maarifa na ujuzi katika kutumia dawa za asili kwa jamii ni muhimu katika kuboresha matumizi ya dawa za asili kwa sasa; na*

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 109 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(f) Maarifa na ujuzi wa dini za asili nchini ni muhimu katika kuabudu na kukuza maadili kwa jamii za sasa.

Tunapaswa kuendeleza asili na urithi wa jamii kwa manufaa ya jamii zetu.

Mbinu za kutumia maarifa na ujuzi wa asili

Jamii ya sasa inaweza kutumia maarifa na ujuzi wa asili katika kuboresha ustawi wake. Jamii ya sasa itawezaje kutumia urithi huu wa maarifa na ujuzi wa asili kwa maendeleo ya sasa?

Kazi za kufanya namba 2



Chunguza na eleza jinsi jamii inayokuzunguka inavyoweza kutumia maarifa na ujuzi wa asili kuboresha ustawi wake.

Jamii zetu zinaweza kutumia maarifa na ujuzi huu wa asili kwa:

(a) Kuboresha shughuli za uchumi za sasa kama vile kilimo, ufugaji, uvuvi, uwindaji, ufinyanzi na ususi wa vitu mbalimbali;

(b) Kuboresha utunzaji wa mazingira ya sasa. Hii itasadia jamii ya sasa kuepuka majanga yatokanayo na uharibifu wa mazingira;

(c) Kuboresha dawa zinazotumiwa na jamii. Pia, kupata dawa zaidi na mbadala za kutibu magonjwa yasiyotibiwa na dawa za kisasa na yale yaliyo sugu;

(d) Kuziboresha dawa za sasa kwa kutumia teknolojia ya sasa ili kuongeza uzalishaji. Hii itaongeza ufanisi na pato la jamii;

(e) Kufanya kazi kwa bidii ili kuendeleza maarifa na ujuzi wa jamii zetu;

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 110 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(f) Kujifunza na kushiriki katika shughuli zilizopo katika jamii zetu ili kuziendeleza; na

(g) Kuhimiza ukuzaji na utunzaji wa asili za jamii ili kuziendeleza kizazi hadi kizazi.

Kusimulia maarifa na ujuzi wa asili, asili za jamii na urithi katika jamii

Kazi ya kufanya namba 3



Fikiri, kisha andika mbinu za kutumia kusimulia maarifa na ujuzi wa asili, asili za jamii na urithi uliopo katika jamii inayokuzunguka.

Tunaweza kutumia mbinu mbalimbali kusimulia maarifa na ujuzi wa asili na urithi wa kihistoria katika jamii inayotuzunguka.

Chunguza Kielelezo namba 1, kisha fanya zoezi linalofuata.



Kielelezo namba 1: *Wanafunzi wakikusanya taarifa za matukio shuleni*

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 111 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Zoezi la 1

1. Orodhesha vifaa vinavyotumika kukusanyia taarifa.
2. Andika vifaa vingine vinavyoweza kutumika kukusanyia taarifa za maarifa na ujuzi wa asili, asili za jamii na urithi uliopo katika jamii zetu.

Tunaweza kuchukua taarifa hizi kwa kutumia vifaa kama kalamu na daftari. Wakati mwingine kamera au simu zinaweza kutumika kupiga picha, kurekodi na kutunza taarifa. Ukusanyaji na utunzaji wa taarifa husaidia kuwa na taarifa sahihi za kusimulia maarifa haya shuleni na nyumbani.

Inatupasa kukusanya taarifa zinazohusu maarifa na ujuzi wa asili, asili za jamii na urithi uliopo katika jamii zetu. Ukusanyaji wa taarifa hizi utawezesha kutambua vitu vya kusimulia. Tunaweza kupata taarifa hizi kwa njia ya masimulizi, uchunguzi au kusoma. Uchunguzi unaweza kufanyika kwa kuwauliza watu wengine kuhusu maarifa na ujuzi wa asili na urithi wa jamii zetu. Pia, tunaweza kutembelea maeneo yenye taarifa hizi; kwa mfano katika makumbusho, maktaba na maeneo yenye hifadhi za nyaraka mbalimbali. Kutembelea maeneo yenye taarifa hizi hutupa nafasi ya kusoma, kuona na kusikiliza taarifa husika. Usomaji wa vitabu, magazeti na majarida yanayohusu maarifa na ujuzi wa asili, asili za jamii na urithi uliopo katika jamii husaidia pia kupata taarifa.

Vilevile, tunaweza kupata taarifa mbalimbali za kusimulia kwa kuuliza na kusikiliza masimulizi kutoka kwa watu waliotuzidi umri kama ilivyo katika Kielelezo namba 2.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 112 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Kielelezo namba 2: *Watoto wakisikiliza masimulizi*

Tunaweza kusimulia taarifa za maarifa na ujuzi wa asili na urithi wa historia katika mikusanyiko mbalimbali. Kwa mfano, tunaweza kusimulia katika paredi za asubuhi na jioni shuleni kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 3.



Kielelezo namba 3. *Mwanafunzi akisimulia jambo katika paredi*

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 113 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Pia, tunaweza kuzisimulia katika vikao vya shule kama ilivyo katika Kielelezo namba 4.



Kielelezo namba 4: *Mwanafunzi akisimulia katika kikao cha shule*

Vilevile, masimulizi haya yanaweza kufanyika darasani kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 5.



Kielelezo namba 5. *Mwanafunzi akisimulia jambo darasani*

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 114 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Tunaweza kuwasimulia wenzetu taarifa hizi katika mazingira yetu pale tunapokuwa pamoja kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 6.



Kielelezo namba 6. *Mwanafunzi akimsimulia mwenzake jambo*

Aidha, masimulizi haya huweza kufanyika kwenye mikutano inayofanyika katika mitaa, vijiji na maeneo ya nyumbani.

Tunaweza kusimulia taarifa zinazohusu asili na urithi wa jamii kwa kuandika ili watu wengine wazisome. Tunaweza kuandika taarifa hizi na kubandika katika kuta za matangazo shuleni. Aidha, taarifa hizi huandikwa kwenye vitabu na magazeti. Hii husaidia watu mbalimbali kusoma na kufahamu kuhusu maarifa na ujuzi huu wa asili na maadili yake. Redio na runinga ni miongoni mwa maeneo yatumikayo pia kusimulia taarifa hizi.

Jamii za kale zilitunga nyimbo na hadithi ambazo hadi sasa zinatupa masimulizi kuhusu maarifa na ujuzi wa jamii na maadili yake.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 115 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Tunaposimulia tunawapa taarifa watu wengine kuhusu maarifa na ujuzi wa asili na urithi tulionao. Bila masimulizi, watu wengine hawawezi kupata taarifa za maarifa na ujuzi wa asili wa jamii zetu.

Zoezi la 2

1. Taja njia nyingine zinazoweza kutumika ili kupata taarifa za maarifa na ujuzi wa asili na urithi wa kihistoria.

Thamani ya asili na urithi wa kihistoria katika jamii

Asili na urithi uliopo umetunza kumbukumbu za jamii zetu.

Kazi ya kufanya namba 4



Fikiri na andika thamani za asili za jamii kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Asili za jamii kama vile tamaduni, mavazi, vyakula, michezo na urithi wa kihistoria vina thamani katika:

(a) Kutambulisha urithi wa kihistoria uliopo katika jamii;
(b) Kutupa ushahidi wa chimbuko la asili za jamii na maadili ya jamii zetu kwa sasa;
(c) Kutoa ushahidi wa asili za tamaduni zetu nchini;
(d) Kupata maarifa na ujuzi wa kutenda maadili katika jamii zetu;
(e) Kupata mapato ya taifa na jamii;
(f) Kupata maarifa na ujuzi wa kujenga misingi ya uzalendo;
(g) Kuendeleza misingi ya maadili ya jamii kama vile umoja, ushirikiano na uhusiano mwema wa kusaidiana katika jamii; na

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 116 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(h) Kutambulisha maadili ya jamii katika utendaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii.

Urithi wa kihistoria na asili za jamii vina thamani kubwa kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa sasa.

Zoezi la jumla

Jibu maswali yafuatayo:

1. Eleza umuhimu wa maarifa na ujuzi wa asili na urithi wa kihistoria kwa maendeleo ya kiuchumi kwa sasa.
2. Eleza umuhimu wa maarifa na ujuzi wa asili na urithi wa kihistoria kwa maendeleo ya kijamii kwa sasa.
3. Orodhesha mbinu tatu (3) tunazoweza kutumia katika kukusanya taarifa kuhusu maarifa na ujuzi wa asili, asili za jamii na urithi wa kihistoria katika mazingira yetu.
4. Eleza mbinu tatu (3) tunazoweza kutumia kusimulia asili za jamii na urithi wa kihistoria.
5. Andika thamani ya asili za jamii na urithi wa kihistoria kwa sasa.

Msamiati

Thamani ubora wa kitu kutokana na hali yake na umuhimu wake

Kusimulia kuelezea, jambo au habari kulingana na mlolongo wa matukio

FOR ONLINE USE ONLY

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 117 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Sura ya Nane

Uhusiano na ushirikiano na jamii

Utangulizi

Katika sura hii utajifunza uhusiano na ushirikiano na watu wanaokuzunguka, nyumbani na shuleni. Pia, utajifunza umuhimu wa uhusiano na ushirikiano wa familia na marafiki zako. Vilevile, utajifunza matendo ya kijamii na kiuchumi yanayojenga uhusiano na ushirikiano katika jamii inayokuzunguka, shuleni na nyumbani. Umahiri utakaoupata utakuwezesha kuwa na uhusiano na ushirikiano mzuri na watu wengine, shuleni na nyumbani.



Fikiri

Uhusiano na ushirikiano na watu wengine.

Uhusiano

Kazi ya kufanya namba 1



Fikiri, kisha andika mambo unayoyafanya na watu unaoishi nao katika familia.

Katika maisha yetu ya kila siku tunaishi na watu mbalimbali, shuleni au nyumbani. Kwa mfano, katika familia tunaishi na wazazi na ndugu wa damu kama baba, mama, kaka na dada. Pia, ndugu wengine wa karibu tunaoweza kuishi nao ni binamu, shangazi, mjomba, bibi na babu.

Vilevile, tuwapo shuleni, kuna watu tunaopenda kuwa nao karibu zaidi ya wengine. Tunapenda kuwa karibu nao kwa

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 118 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

sababu mbalimbali, ikiwemo kucheza na kusoma pamoja. Aidha, tunapenda kuwa nao karibu kwa sababu wanatusikiliza, wanatupenda, wanatusaidia na wanatujali zaidi ya watu wengine. Mara nyingi, ndio watu tunaopenda kutembea na kukaa nao pamoja zaidi ya watu wengine. Vilevile, ni watu tunaopendelea kuwapa zawadi zaidi ya watu wengine. Mara nyingi ni vigumu kujenga ukaribu na watu ambao tunatofautiana kitabia na mitazamo yetu. Hata hivyo, kadri tunavyokuwa karibu ndivyo tunavyojenga uhusiano. Uhusiano hujengwa kwa kukutana mara kwa mara, kufahamiana au kuwa karibu na watu wengine, nyumbani au shuleni.

Uhusiano huelezea jinsi watu wanavyofahamiana na kushirikiana katika mazingira tofauti. Uhusiano hupelekea watu kujenga ukaribu na mshikamano baina yao. Uhusiano unaweza kuwa wa kirafiki au kifamilia.

Uhusiano wa kifamilia

Uhusiano na familia ni aina ya uhusiano ambao unajumuisha wazazi na ndugu wa damu kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 1.



Kielelezo namba 1: *Baba, mama na watoto katika familia*

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 119 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Uhusiano wa familia ni wa asili, kwani mwanadamu anaupata kwa kuzaliwa. Uhusiano huu unajengwa kwa uhusiano wa damu. Mtu hujikuta tu ana uhusiano na watu wa familia yake kwa kuzaliwa katika familia hiyo. Pia, uhusiano huu wa familia hujengwa kwa sababu ya ndoa, pale mtu mume na mke wanapofunga ndoa.

Chunguza mti wa familia, kisha fanya zoezi la 1.



Kielelezo namba 2: *Mti wa familia*

Zoezi la 1

1. Andika kwenye mti wa familia
   (a) Jina la baba yako.
   (b) Jina la mama yako.
   (c) Kama una kaka, jina la kaka yako au kaka zako.
   (d) Kama una dada, jina la dada yako au dada zako.

Watu tulioandika majina yao ni watu ambao huwa karibu nasi katika familia kila siku. Uhusiano wa kifamilia ni uhusiano wa maisha yote. Wanafamilia wanatakiwa kupendana, kuheshimiana, kushirikiana, kuwa karibu na kusaidiana.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 120 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Vilevile, uhusiano wa kifamilia huhusisha watu wa karibu; kwa mfano, babu, bibi, shangazi, mjomba na binamu. Kielelezo namba 3 kinaonesha uhusiano wa kifamilia na ndugu wa karibu.



Kielelezo namba 3: *Uhusiano wa wazazi, watoto, babu, bibi mjomba na shangazi*

Chunguza kielelezo namba 4 kuhusu mti wa ndugu wa karibu na familia, kisha fanya zoezi la 2.



Kielelezo namba 4: *Mti wa ndugu wa karibu na familia*

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 121 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Zoezi la 2

1. Andika majina ya ndugu wafuatao katika visanduku vilivyopo katika Kielelezo namba 4.
   (a) Wazazi wa mama na baba (bibi na babu).
   (b) Kaka zake na wadogo zake mama na baba.
   (c) Dada zake na wadogo zake mama na baba.
   (d) Watoto wa dada zake na wadogo zake mama na baba (binamu).
   (e) Watoto wa kaka zake na wadogo zake mama na baba (binamu).

Matendo ya kuhusiana katika familia

Tunapaswa kutenda matendo ya kuhusiana ili kukuza uhusiano katika familia.

Chunguza picha hizi, kisha fanya zoezi linalofuata.



Kielelezo namba 5: *Matendo ya uhusiano katika familia*

Zoezi la 3

1. Je, ni matendo gani unayoyaona katika picha hizi?
2. Kitu gani umejifunza kutokana na picha hizi?
3. Eleza matendo mengine ya kuhusiana katika familia?

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 122 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Tunaweza kufanya matendo ya kuhusiana na jamaa wa karibu na familia ili kujenga uhusiano mzuri kati yetu na wao.

Kazi ya Kufanya namba 2



Waulize wazazi au walezi kuhusu matendo ambayo familia yako huyafanya ili kujenga uhusiano mzuri na ndugu wa karibu na familia yenu.

Tunaweza kujenga uhusiano na watu wa familia na ndugu wa karibu na familia kwa kuwatembelea mara kwa mara. Kutembeleana hujenga uhusiano wa karibu na upendo na ndugu wa karibu. Kutembelea ndugu wa karibu ni vitendo vya maadili ya Kitanzania.

Pia, tunaweza kushirikiana na wanafamilia katika matukio kama vile sherehe na misiba, pale inapotokea kwa ndugu zetu wa karibu. Vilevile, uhusiano huu unaweza kujengwa kwa kushirikishana mambo mbalimbali ya kuleta maendeleo. Tangu kale, jamaa wa karibu walishirikiana katika mambo ya kimaendeleo ili kujenga uhusiano wa karibu na familia na jamii.

Uhusiano wa kirafiki

Uhusiano wa kirafiki hujengwa kati ya watu wanaowasiliana au kushirikiana mara kwa mara. Mawasiliano ya mara kwa mara husababisha watu kufahamiana kitabia, kimwenendo na mitazamo; na hivyo, kujenga urafiki. Uhusiano ukijengwa husababisha ukaribu baina ya watu wawili au zaidi.

Chunguza Kielelezo namba 6, kisha jibu maswali katika zoezi linalofuata.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 123 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

A.



B.



Kielelezo namba 6: *Matendo ya uhusiano mzuri na marafiki*

Zoezi la 4

1. Andika matendo ya uhusiano yaliyopo katika picha A na B.
2. Eleza matendo mengine yanayojenga uhusiano wa kirafiki.

Kujenga uhusiano wa kirafiki na watu wengine ni muhimu. Zipo njia mbalimbali za kujenga uhusiano na marafiki zetu, shuleni au nyumbani. Tunaweza kujenga uhusiano wa kirafiki kwa kucheza pamoja. Pia, tunaweza kujenga uhusiano wa kirafiki kwa kusoma pamoja, kupeana zawadi, kula na kufanya kazi pamoja. Angalia mfano katika Kielelezo namba 7.



Kielelezo namba 7:
Wanafunzi wakipeana zawadi

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 124 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kupeana zawadi husaidia kukuza upendo kati ya marafiki na huimarisha uhusiano. Uhusiano na marafiki ni muhimu sana katika maisha yetu ya kila siku. Uhusiano mzuri wa kirafiki hujenga mazingira ya kusaidiana, kujifunza kutoka kwa wengine na kuleta ufanisi katika mambo tunayoyafanya.

Pamoja na umuhimu wa kujenga urafiki, ni vema kujenga uhusiano unaofaa. Kabla ya kujenga uhusiano ni vema kufahamiana vyema. Hii itasaidia kuepuka marafiki ambao wanaweza kusababisha tukajiingiza katika vitendo ambavyo ni kinyume na maadili ya jamii.

Kazi za kufanya namba 3



Fikiri na andika athari za kujenga uhusiano wa kirafiki usiofaa.

Urafiki huathiri tabia za vijana iwapo kuna tofauti kati yao katika vitendo, malezi, makuzi na mienendo. Uchaguzi wa marafiki wema na wenye tabia nzuri unapaswa kusisitizwa katika kujenga na kukuza uhusiano wa kirafiki.

Umuhimu wa uhusiano wa familia na marafiki

Kazi ya kufanya namba 4



Andika umuhimu wa uhusiano wa kifamilia na marafiki wengine nyumbani na shuleni.

Uhusiano ni muhimu katika maisha ya binadamu.

Katika familia, uhusiano:

(a) Husaidia kujenga msingi imara wa upendo, maelewano, na kupata msaada kutoka kwa ndugu wa karibu; na

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 125 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Huwa chanzo cha faraja, usalama, na utulivu. Watu wanaoungwa mkono na familia zao wanakuwa na uwezo mkubwa wa kukabiliana na changamoto za maisha.

Katika urafiki, uhusiano:

(a) Huleta furaha kwa watu wanaohusiana. Kwa mfano, urafiki mzuri unaweza kuleta hisia za usalama na kujisikia kuwa na mtu wa kuzungumza naye wakati wa shida;

(b) Husaidia katika kufikia malengo yetu binafsi. Kwa mfano, mwanafunzi anaweza kupata msaada kutoka kwa rafiki yake katika kufikia malengo yake ya kimasomo; na

(c) Hujenga mazingira ya kusaidiana katika hali mbalimbali.

Zoezi la 5

1. Eleza hasara za kuwa na uhusiano mbaya na watu wa familia.
2. Eleza hasara za kukosa uhusiano wa kirafiki.

Matendo ya kijamii ya kujenga ushirikiano na uhusiano na jamii

Katika mazingira yetu, tunaishi na watu wengine mbali na familia zetu. Watu hawa tunaishi nao katika mtaa au kijiji kimoja kama majirani zetu. Watu hawa ni muhimu sana kwetu, hivyo, ni muhimu kujenga uhusiano mzuri kati yetu na wao.

Kazi ya kufanya namba 5



Waulize wazazi au walezi mambo ambayo familia yako hushirikiana na majirani zenu nyumbani.

Tunapaswa kutenda matendo ya kijamii ili kujenga uhusiano na watu wanaotuzunguka. Matendo ya kijamii tunayoweza

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 126 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kufanya ili kujenga uhusiano katika jamii ni kusaidiana kwenye shida mbalimbali kama vile msiba, ugonjwa na majanga. Kutembelea na kuhudumia wagonjwa ni matendo mengine ya kijamii yanayojenga uhusiano mzuri katika jamii. Unaposhiriki katika matendo haya katika jamii, unajenga uhusiano mwema na majirani zako. Pia, hutoa nafasi ya kusaidiwa na jamii pale na wewe unapopatwa na tatizo.

Tangu kale, jamii zilisisitiza uhusiano na jamii inayotuzunguka. Uhusiano huu ulijengwa kwa wanajamii kushiriki katika michezo na sherehe mbalimbali. Kwa mfano, jamii zilishiriki katika michezo kama vile bao, mieleka, masumbwi na ngoma. Ushiriki huu uliwasaidia watu katika jamii na hata jamii za karibu kufahamiana na kujenga uhusiano wa karibu. Pia, sherehe mbalimbali, kama vile za mavuno, jando na unyago zilifanyika ili kujenga uhusiano. Vilevile, jamii zilikuwa na siku rasmi ya soko (gulio) ambapo watu kutoka katika jamii za karibu na eneo la gulio walikusanyika kwa ajili ya kuuza na kununua vitu na mazao. Siku za gulio zilikuwa rasmi. Jamii ilishiriki kwa ajili ya kuuza na kununua vitu mbalimbali. Ushiriki katika gulio ulisaidia watu kufahamiana na kujenga uhusiano wa karibu.

Hata sasa, jamii zetu zinaweza kuendeleza uhusiano wa kijamii. Shuleni, wanafunzi wanaweza kukuza uhusiano kwa kushiriki shughuli za usafi kama vile kufagia, kufyeka nyasi, kukatia miti na maua, kusafisha darasa na kumwagilia maua. Pia, kushiriki katika shughuli za kitaaluma kama vile, kusoma pamoja ni sehemu ya kukuza uhusiano kati yetu. Ushiriki huu unaweza kusaidia kujenga uhusiano kati yetu na watu wengine shuleni. Vilevile, shule zinaweza kukuza uhusiano kwa kushirikiana katika masuala ya kitaaluma na michezo. Shule zinapofanya mashindano katika michezo na taaluma hukuza uhusiano kati yao.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 127 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Nyumbani, tunaweza kujenga na kuendeleza uhusiano na majirani zetu kwa kushiriki katika sherehe kama sherehe za harusi na sherehe za dini. Pia, kushiriki katika vikao na michezo kama inavyooneka kwenye Kielelezo namba 8 hujenga uhusiano katika jamii.



Kielelezo namba 8: *Kushiriki michezo katika jamii*

Vilevile, tunapaswa kushiriki katika ulinzi na kutoa taarifa ya vitendo vinavyoharibu usalama wa jamii zetu. Ushiriki huu husaidia kujenga usalama na uhusiano katika jamii.

Kazi ya kufanya namba 6

Chunguza na andika mambo mengine tunayoweza kushirikiana ili kujenga uhusiano katika jamii zinazotuzunguka.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 128 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Matendo ya kiuchumi ya kujenga ushirikiano na uhusiano na jamii

Uhusiano katika jamii hujengwa kwa kushiriki katika shughuli za kiuchumi. Tangu kale, jamii zilijenga uhusiano kati ya jamii na jamii katika shughuli za biashara, kilimo, uwindaji, uvuvi na kadhalika. Katika biashara, uhusiano ulianza kati ya familia na familia, ambapo zilibadilishana vitu na mazao ili kukidhi mahitaji ya kifamilia. Baadae, uhusiano ulikua kati ya ukoo na ukoo, hata jamii na jamii. Uhusiano katika kubadilishana vitu na mazao ulikuwa muhimu kwani uliwasaidia watu kupata chakula na mahitaji mengine yaliyokosekana katika maeneo yao. Kwa mfano, jamii za wakulima zilibadilishana chakula na vyungu, chumvi na majembe kutoka katika jamii zingine. Pia, wafugaji walibadilishana maziwa au mifugo kwa nafaka kutoka kwa wakulima. Vilevile, wavuvi walibadilishana samaki kwa nafaka kutoka kwa majirani zao ambao ni wakulima. Hii iliimarisha uhusiano kati ya familia, ukoo, na jamii; huu ndio mwanzo wa kukua kwa biashara katika jamii za Kitanzania. Kukua kwa teknolojia za asili, kama vile ugunduzi wa chuma, kulisaidia kuimarika kwa shughuli za uchumi katika jamii, hata kukawa na uzalishaji wa ziada wa mazao na vifaa vilivyotengenezwa kwa chuma. Maendeleo haya yalisaidia jamii kuwa na ziada na kuongeza uhitaji wa kubadilishana vitu mbalimbali kati ya jamii moja na zingine. Hivyo, uhusiano kati ya jamii na jamii ulizidi kukua.

Aidha, jamii za kale zilishirikiana katika shughuli zingine za uchumi kama vile kilimo, ufugaji na uvuvi. Watu walialikwa wakati wa kilimo kuisaidia jamii fulani kulima, kupalilia na kuvuna mazao. Watu walipoalikwa walikwenda kushiriki bila kudai malipo yoyote. Watu walifanya kazi kwa pamoja na baada ya kazi walikula na kupumzika pamoja huku wakiimba nyimbo na kucheza ngoma. Licha ya uhusiano huu kujenga uchumi, ulisaidia pia kujenga na kuendeleza uhusiano kati ya wanajamii.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 129 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kazi ya kufanya namba 7

Chunguza matendo ya kiuchumi ambayo jamii wanashirikiana katika maeneo yanayokuzunguka.

Uhusiano katika jamii kwa sasa unaweza kujengwa kwa kushirikiana katika shughuli mbalimbali za uchumi kama vile kilimo, uvuvi na ujenzi kama ilivyokuwa hapo kale. Hii ni muhimu kwani, licha ya ushirikiano huu kuleta maendeleo katika jamii, husaidia pia kujenga uhusiano mwema.

Vilevile, jamii zetu kwa sasa zinaweza kujenga uhusiano kwa kushiriki katika shughuli za kiuchumi katika jamii zetu. Shughuli za kiuchumi tunazoweza kushiriki ni kama kilimo, ufugaji, uvuvi na biashara. Kwa mfano, watu wanaweza kushiriki katika ujenzi wa shule, zahanati na miundo mbinu mingine katika maeneo yanayowazunguka kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 9.



Kielelezo namba 9: *Wanajamii wakishiriki shughuli za ujenzi*

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 130 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Watu wanaweza kushirikiana kwa kufanya kazi kwa pamoja ili kufikia malengo waliojiwekea. Aidha, wanaweza kushiriki katika matendo ya uchumi kwa kununua mazao na vitu vingine vya biashara kutoka kwa wanajamii wanaowazunguka. Tunaweza kununua vitu sokoni, dukani au mashambani kutoka kwa majirani zetu. Pia, tunaweza kushiriki katika vikao vya maendeleo katika jamii zetu na kutoa michango ya fedha, vifaa au nguvu kufanikisha shughuli za maendeleo kwenye maeneo yanayotuzunguka. Matendo haya yatasaidia kujenga na kukuza uhusiano na watu wanaotuzunguka. Hivyo, kushiriki katika shughuli za kiuchumi hujenga uhusiano mwema katika jamii.

Kazi ya kufanya namba 8



Andika matendo mengine ya kiuchumi yanayodumisha ushirikiano na uhusiano na watu wengine katika jamii.

Tunapaswa pia kutenda matendo ya kujenga uhusiano wa urafiki na watu wengine. Uhusiano mwema katika jamii hujenga maadili mema. Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye uhusiano mzuri kati ya jamii na jamii. Uhusiano na ushirikiano katika jamii umewasaidia watu kuishi kwa upendo na amani. Amani na upendo tulionao ni matokeo ya uhusiano na ushirikiano uliopo miongoni mwetu Watanzania. Jamii ya sasa inapaswa kudumisha na kuendeleza uhusiano mwema ambao ulikuwepo katika jamii za Watanzania tangu kale. Uhusiano mwema utasaidia jamii ya sasa kujenga umoja na upendo katika jamii na kuondoa ubaguzi. Uhusiano mwema ni chanzo cha maendeleo.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 131 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Zoezi la jumla

1. Orodhesha shughuli tatu (3) za kiuchumi zinazojenga uhusiano katika jamii.
2. Orodhesha matendo matatu (3) ya kijamii yanayojenga uhusiano katika jamii yako.
3. Eleza tofauti kati ya uhusiano wa kifamilia na kirafiki.
4. Eleza mambo ya kuzingatia katika kuchagua marafiki.
5. Eleza mbinu za kuimarisha uhusiano na ndugu wa karibu na familia.
6. Eleza umuhimu wa uhusiano wa kirafiki.
7. Elezea mambo ya kujenga uhusiano mzuri na watu wanaokuzunguka.

Msamiati

Jamaa watu wenye uhusiano fulani wa kindugu

FOR ONLINE USE ONLY

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 132 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Sura ya Tisa

Kukuza na kutunza maadili ya jamii

Utangulizi

Katika sura hii utajifunza kuhusu dhana ya ukuzaji na utunzaji wa maadili. Utajifunza nafasi ya mifumo ya uongozi katika ngazi ya familia, ukoo na shule na mchango wao katika ukuzaji na utunzaji wa maadili. Pia, utajifunza kuhusu misingi ya ukuzaji na utunzaji wa maadili ya jamii. Vilevile, utajifunza kuhusu wajibu wa jamii katika kukuza na kutunza maadili. Umahiri utakaoupata katika sura hii utakuwezesha kukuza na kutunza maadili katika mazingira yanayokuzunguka.



Fikiri

Kukuza na kutunza maadili ya jamii.

Dhana ya kukuza na kutunza maadili

Maadili huelezea taratibu, kanuni na sheria za kuishi ili kuendana na jamii husika. Maadili ya jamii huwekwa na jamii na hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kila kizazi kina wajibu wa kukuza na kutunza maadili ya jamii yao.

Kazi ya kufanya namba 1



Fikiri, andika kisha washirikishe wenzako namna ya kukuza na kutunza maadili katika jamii inayotuzunguka.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 133 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Tunakuza maadili kwa kutenda matendo ya kimaadili. Matendo ya kukuza maadili hufanyika kwa kuzingatia kanuni, taratibu na sheria za jamii husika. Tunatunza maadili kwa kusimamia utendekaji wa maadili katika jamii. Ukuzaji na utunzaji wa maadili ni matendo ya kutenda, kusimamia na kudumisha maadili katika jamii husika.

Zoezi la 1

Soma matendo yaliyoorodheshwa **sehemu A**, kisha ainisha kwa kuandika matendo ya kimaadili katika **sehemu B** na yasiyo ya kimaadili katika **sehemu C.**

A	B	C
Matendo	Matendo ya kimaadili	Matendo yasiyo ya kimaadili
kuwaheshimu watu waliotuzidi umri, kupigana na watu wengine, kuvaa nguo fupi na zinazobana, kuiba, kushirikiana na watu wengine, kutowajali watu wengine, kusema uongo, kuwathamini watu wengine, kusalimiana na wenzako		

Kazi ya kufanya namba 2



Andika watu wanaosimamia matendo ya kimaadili nyumbani.

Mfumo wa uongozi katika ukuzaji na utunzaji wa maadili

Familia, ukoo, shule na jamii zina mifumo mbalimbali ya uongozi ya kusimamia ukuzaji na utunzaji wa maadili.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 134 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Tangu kale, jamii zetu ziliweka mifumo imara katika ngazi mbalimbali ili kuimarisha ukuzaji na utunzaji wa maadili ya jamii. Viongozi katika ngazi zote walishirikiana katika kukuza na kutunza maadili ya jamii.

Kazi ya kufanya namba 3



Chunguza na eleza mifumo ya uongozi inayotumika katika kukuza na kutunza maadili katika ngazi ya familia, ukoo na shule.

Mfumo wa ukuzaji na utunzaji wa maadili katika familia

Katika familia, wazazi, baba na mama, wana jukumu la kuwalea watoto wao. Malezi ya mtoto ni pamoja na kumfundisha maadili mema. Pia, wazazi wana jukumu la kusimamia na kuhakikisha kuwa kila mmoja katika familia anatenda matendo ya maadili ya jamii.

Kazi za kufanya namba 4



Fikiri, andika na washirikishe wenzako mambo matano (5) ya kimaadili uliyofundishwa na wazazi au walezi nyumbani.

Wazazi au walezi ndio kitovu cha ukuzaji na utunzaji wa maadili katika jamii. Pia, watu waliotuzidi umri, kaka na dada zetu katika familia, wana wajibu huo. Wazazi na walezi huwafundisha watoto wao maadili ya jamii kwa vitendo, mifano au masimulizi. Mara nyingine, watoto hujifunza kwa kuiga matendo ya kimaadili kutoka kwa wazazi au walezi wao.

Hivyo, wazazi na walezi wana jukumu la kutenda matendo mema ili watoto wao waone, wasikie na waige matendo hayo. Wazazi au walezi kufanya matendo yasiyofaa mbele

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 135 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ya watoto wao ni makosa. Hii ni kwa sababu watoto huiga matendo hayo.

Pia, wazazi na walezi wana jukumu la kusimamia utunzaji wa maadili katika familia. Mtoto anapofanya vitendo visivyo vya kimaadili, wazazi wana wajibu wa kuhakikisha mtoto anabadilika kwa kutenda matendo ya kimaadili. Wazazi na walezi hutoa adhabu au onyo ili kuzuia tabia mbaya. Tangu kale, wazazi walikuwa ndio kiini cha ukuzaji na utunzaji wa maadili kwenye familia zao.

Mfumo wa uongozi wa ukoo katika ukuzaji na utunzaji wa maadili

Tangu kale, watu wa jamaa moja walikuwa na mifumo imara ya kukuza maadili ya jamii. Wazazi walishirikiana na jamaa wa karibu katika ukoo kutunza maadili ya jamii. Ukoo ulichagua kiongozi ili kusimamia na kutunza maadili. Kiongozi huyu ndiye alikuwa na jukumu la kusimamia mambo yote ya ukoo.

Kazi ya Kufanya namba 5



Andika jina la kiongozi wa ukoo wako anayesimamia ukuzaji na utunzaji wa maadili.

Kiongozi wa ukoo ndiye alikuwa na jukumu la kusimamia maadili na changamoto za kimaadili katika ukoo. Mifumo ya uongozi wa ukoo katika kusimamia maadili ya koo zao imesaidia kutunza maadili ya jamii na kuleta ustawi wa jamii zetu.

Kazi ya kufanya namba 6



Fikiri na andika mambo matano (5) ya kimaadili uliyofundishwa na ndugu wa karibu katika ukoo.

Ukuzaji na utunzaji wa maadili katika koo zetu hufanywa kwa kushirikiana na ndugu wa karibu kama vile babu, bibi, mjomba,

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 136 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

shangazi na ukoo mzima. Hawa wote wana wajibu mkubwa wa kukuza na kutunza maadili ya jamii zetu.

Mbinu za kukuza na kutunza maadili

Jamii kwa ujumla ilishirikiana katika kukuza na kutunza maadili. Mtu yeyote aliyemkuta mtoto akifanya matendo yasiyokubalika katika jamii alimpa adhabu na alitoa taarifa. Wazazi walipopata taarifa walimwadhibu tena mtoto wao ili kuimarisha umoja katika kukuza na kutunza maadili. Hii ilisaidia sana kukuza maadili yetu. Mfumo huu wa malezi ulisababisha woga katika kipindi hicho. Hakuna aliyethubutu kufanya tabia mbaya mbele ya mtu yeyote kwani watu waliogopa kuadhibiwa.

Wakati mwingine, wazazi waliongozana na watoto katika sherehe na misiba ili kuwapa nafasi watoto kujifunza maadili katika kushiriki kwenye matukio ya kijamii. Pia, kulikuwa na watu rasmi katika ukoo, kwa mfano mjomba, shangazi, mama mkubwa na mdogo, ambao walitumika katika kufundisha maadili fulani. Vilevile, jamii ilichagua watu rasmi wa kufundisha maadili na afya ya uzazi kutoka kizazi kimoja hadi kingine wakati wa jando na unyago kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 1 na 2.



Kielelezo namba 1. *Watoto wa kiume wakifundishwa maadili jandoni*

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 137 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Kielelezo namba 2. *Watoto wa kike wakifundishwa maadili unyagoni*

Njia za masimulizi zilitumika kufundisha tabia njema na kuonya tabia mbaya. Pia, vitendawili, methali, mafumbo na misemo ilitumika kuwafundisha watoto maadili ya jamii zetu. Angalia mfano katika Kielelezo namba 3.



Kielelezo namba 3: *Mzee akiwafundisha wajukuu zake maadili*

Zoezi la 2

1. Eleza mafunzo yaliyopo katika methali zifuatazo katika kukuza na kutunza maadili:
   (i) Asiyesikia la mkuu huvunjika guu;

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 138 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(ii) Samaki mkunje angali mbichi;
(iii) Usiache mbachao kwa msala upitao; na
(iv) Kikulacho ki nguoni mwako.

2. Andika methali nyingine mbili (2) zenye mafunzo ya kimaadili.
3. Eleza mafunzo ya kukuza na kutunza maadili tunayopata katika misemo ifuatayo:
   (i) Mtegemea cha nduguye hufa maskini; na
   (ii) Mwenda bure si sawa na mkaa bure.
4. Andika misemo mingine miwili (2) yenye mafunzo ya kukuza na kutunza maadili.
5. Andika vitendawili viwili (2) vyenye mafunzo ya kimaadili.

Vilevile, nyimbo zilitungwa na ngoma zikachezwa katika sherehe ili kufunza maadili ya jamii. Watu waliposikiliza nyimbo walipata ujumbe na kujirekebisha pale walipokosea. Nyimbo hizi zilisisitiza tabia njema na hata kukemea tabia mbaya. Maarifa na ujuzi katika sanaa vilitumika kukuza na kutunza maadali yetu. Haya yote yaliwasaidia watu kutambua, kufahamu na kuthamini maadili ya jamii.

Kazi ya kufanya namba 7



Jadili namna muziki wa kizazi kipya, katuni, tamthilia, simu janja na matangazo yanavyochangia katika kuharibu na kukuza maadili nchini kwa sasa.

Aidha, imani katika dini zilitumika kukuza na kutunza maadili. Watu waliamini matukio mabaya katika koo hutokea kwa kukiuka matendo mema katika jamii. Koo ziliamini kuwepo kwa Mungu ambaye anatoa adhabu iwapo kutatokea vitendo vya kukiuka maadili. Imani ya dini iliwafanya watu kutenda matendo mema. Mila na desturi hizi zilikuzwa na kutunzwa kizazi hadi kizazi.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 139 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Miiko mbalimbali iliwekwa ili kusimamia na kutunza maadili ya jamii husika. Miiko hii ilionya na kukataza tabia fulani ili kukuza na kutunza maadili ya jamii husika.

Kazi ya kufanya namba 8



Waulize wazazi au walezi wako kuhusu miiko iliyowekwa katika jamii yako ili kukuza na kutunza maadili katika jamii.

Mfumo wa uongozi wa shule katika ukuzaji na utunzaji wa maadili

Kama ilivyo katika familia na ukoo, shule pia ina mfumo imara wa ndani na nje katika ukuzaji na utunzaji wa maadili. Mfumo wa uongozi wa shule unahusisha walimu na jamii (chunguza Kielelezo namba 4).



Kielelezo namba 4: *Mfumo wa uongozi katika ngazi ya shule*

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 140 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kazi ya kufanya namba 9



Chunguza mfumo wa uongozi katika Kielelezo namba 4 na andika majukumu ya kila ngazi ya uongozi wa shule katika kukuza na kutunza maadili shuleni.

Viongozi wa shule husimamia maadili kwa kushirikiana na jamii, walimu na wanafunzi.

Zoezi la 3

1. Eleza nani mwenye jukumu la kuchukua hatua za usimamizi wa maadili iwapo itatokea:
   (i) Kuchelewa kufika shuleni _____
   (ii) Kupiga kelele darasani _____
   (iii) Kumtukana mwalimu _____
   (iv) Kutokumaliza kazi za masomo darasani _____
   (v) Kutokuvaa sare za shule _____
   (vi) Kukosa vipindi darasani _____
   (vii) Kupigana na mwalimu _____
   (viii) Kupigana na mwenzako shuleni _____
   (ix) Kuwatukana wengine _____
   (x) Kuwasukuma au kufinya wengine _____

Kuna viongozi wanaosimamia ukuzaji na utunzaji wa maadili shuleni.

Mwalimu mkuu

Mwalimu mkuu ndiye kiongozi mkuu katika ngazi ya shule. Mwalimu mkuu ana jukumu la kusimamia mambo ya taaluma na nidhamu za wanafunzi wote shuleni. Pia, ana jukumu la kukuza maadili mema kwa wanafunzi. Kwa mfano, kusimamia maendeleo ya taaluma, utii wa sheria na taratibu za shule pamoja na kutuza rasilimali za shule.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 141 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Walimu

Shule ina walimu wenye majukumu ya kiuongozi katika kufuatilia maadili na taaluma shuleni katika ngazi mbalimbali. Kwa mfano, mwalimu wa darasa ana jukumu la kukuza maadili katika darasa analolisimamia. Pia, kuna mwalimu wa nidhamu. Mwalimu huyu ndiye kiongozi mkuu wa kusimamia maadili shuleni. Walimu wote kwa pamoja wana jukumu la kukuza maadili shuleni kwa kuwafundisha wanafunzi jinsi ya kufanya matendo mema ya kimaadili. Matendo hayo ni kama vile kutii kanuni za shule na za darasani pamoja na kuwaheshimu na kujali watu wengine shuleni.

Kazi za kufanya namba 10



Andika majukumu ya mwalimu wa darasa na mwalimu wa nidhamu katika kukuza na kutunza maadili shuleni.

Viongozi wa wanafunzi

Uongozi wa wanafunzi wa shule unajumuisha viranja wa shule na wa darasani. Viongozi hawa wanawaongoza wanafunzi wengine katika kukuza na kutunza maadili mema. Kwa mfano, kuwasimamia wanafunzi wenzao kuwahi shuleni. Pia, kiranja huandika majina ya waliochelewa kufika shuleni. Vilevile, huandika majina ya wanafunzi ambao hawakufanya usafi katika maeneo yao. Aidha, kiranja huhakikisha wanafunzi wenzake hawapigi kelele darasani. Viongozi wa wanafunzi hutoa taarifa kwa walimu, hasa mwalimu wa zamu na wa darasa iwapo kuna tatizo la ukiukwaji wa maadili shuleni.

Kamati ya shule

Kamati ya shule huongozwa na wazazi ambao huchaguliwa na wazazi wenye watoto katika shule husika. Kamati ya shule ina jukumu la kukuza na kutunza maadili katika shule.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 142 27/11/2023 12:19

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Pia, kamati hii husimamia maadili ya wanafunzi na walimu shuleni.

Kazi ya kufanya namba 11



Andika majukumu ya kamati ya shule katika kukuza na kutunza maadili mema kwa wanafunzi na walimu shuleni.

Misingi ya ukuzaji na utunzaji wa maadili ya jamii

Jamii zilikuwa na misingi ya ukuzaji na utunzaji wa maadili. Misingi hiyo ilisisitiza uadilifu, haki, usawa na uwazi katika kukuza na kutunza maadili ya jamii.

Kazi ya kufanya namba 12



Tafuta na andika maana ya maneno uadilifu, haki, umoja, usawa na uwazi kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo tovuti na maktaba mtandao.

Uadilifu

Ukuzaji na utunzaji wa maadili ulizingatia misingi ya uadilifu. Watu waliosimamia maadili walikuwa wawazi, wakweli na watenda haki kwa watu wote. Hapakuwa na upendeleo. Kila mtu alipewa onyo au adhabu kwa usawa kulingana na kosa husika. Misingi hii ilisaidia kuwepo kwa uaminifu na heshima pale viongozi wa jamii waliposisitiza na kusimamia utekelezaji wa maadili ya jamii.

Haki na usawa

Misingi ya haki na usawa pia ilizingatiwa katika ukuzaji na utunzaji wa maadili. Misingi hii ilisaidia kumpa kila mtu stahiki na haki yake bila upendeleo. Usawa katika kupata haki ulizingatiwa bila kujali hali ya mtu.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 143 27/11/2023 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Uwazi

Ukuzaji na utunzaji wa maadili vilifanyika katika misingi ya uwazi. Hii iliwasaidia watu kutambua na kujifunza matendo mema na athari za matendo mabaya. Pia, iliwasaidia watu wengine kutambua njia sahihi za kukuza na kutunza maadili ya jamii. Aidha, uwazi uliwasaidia watu kufichua matendo maovu yanayoendelea kwenye jamii yao. Tatizo la kimaadili lilijadiliwa kwa uwazi na familia kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 5.



Kielezo namba 5: *Wazazi na watoto wakizungumza kwa uwazi*

Hali hii iliondoa upendeleo na ukweli ulijulikana. Adhabu zilitolewa kwa uwazi ili watu wote watambue athari za tabia mbaya. Hii ilisaidia kukuza na kutunza maadili ya familia, ukoo na jamii.

Umoja

Ukuzaji na utunzaji wa maadili ulifanyika kwa umoja. Jamii nzima ilishirikiana katika kukuza na kutunza maadili. Jamii nzima ilikubaliana katika kanuni, sheria na taratibu za jamii zao. Hivyo, kila mmoja aliwajibika kuzifuata na kuzilinda. Hapakuwa na mtu aliyetenda kinyume na maadili ya jamii yake.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 144 27/11/2023 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kazi ya kufanya namba 13



Chunguza na andika namna misingi ya uadilifu, haki, usawa, umoja na uwazi inavyozingatiwa katika ukuzaji na utunzaji wa maadili nyumbani na shuleni.

Misingi ya ukuzaji na utunzaji wa maadili inapaswa kuzingatiwa kwa sasa ili kuleta usawa katika jamii. Hii itasaidia jamii kukuza na kutunza maadili kwa sasa.

Kazi ya kufanya namba 14



Andika mambo uliyojifunza kuhusu mfumo wa uongozi katika ukuzaji na utunzaji wa maadili.

Wajibu wa jamii katika kukuza na kutunza maadili

Tangu kale hadi sasa, jamii ina wajibu wa kukuza na kutunza maadili yake. Tunaweza kutumia njia mbalimbali katika kukuza na kutunza maadili ya jamii zetu.

Kazi ya kufanya namba 15



Fikiri, andika na washirikishe wenzako kuhusu wajibu wako katika kukuza na kutunza maadili nyumbani na shuleni.

Tuna wajibu wa kufanya yafuatayo ili kukuza maadili:

(a) Kuwafundisha wengine tabia njema. Tunaweza kuwafundisha watu wengine maadili kwa kuwaeleza matendo ya kimaadili ya jamii zetu. Haya yanaweza kufanyika maeneo ya nyumbani na shuleni;

(b) Kuishi kwa kuzingatia maadili na kuwahimiza watu wengine kutenda matendo ya kimaadili na kuacha kukiuka maadili ya jamii; na

(c) Kuacha kuiga vitendo vilivyo kinyume na maadili.

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 145 27/11/2023 12:20

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Tuna wajibu wa kufanya yafuatayo ili kutunza maadili:

(a) Kutenda matendo ya kimaadili nyumbani na shuleni;

(b) Kutoa taarifa iwapo kuna matendo yanayokiuka maadili nyumbani na shuleni; na

(c) Kusimamia na kusisitiza maadili yanayokubalika katika mazingira yanayotuzunguka.

Zoezi la jumla

1. Andika mambo matatu (3) uliyojifunza kuhusu ukuzaji na utunzaji wa maadili.
2. Eleza majukumu mawili (2) ya viongozi wa familia na ukoo katika kukuza na kutunza maadili.
3. Eleza mbinu zilizotumiwa na jamii za kale katika kukuza na kutunza maadili.
4. Eleza faida mbili (2) za ushiriki wa jamii nzima katika kukuza na kutunza maadili ya jamii.
5. Eleza hasara mbili (2) za familia kukuza na kutunza maadili ya mtoto peke yake bila ushiriki wa jamii nzima.
6. Eleza mambo ya kufanya kwa sasa ili kukuza na kutunza maadili.

Msamiati

Koo familia au jamaa zenye uhusiano wa damu

Mfumo utaratibu uliowekwa na kutambuliwa kwa kusudi fulani

Misingi mambo muhimu yanayounda jambo fulani

Uongozi madaraka aliyonayo mtu katika kusimamia watu wengine

Historia ya Tanzania na Maadili STD 3 PB Final.indd 146 27/11/2023 12:20

Taasisi ya Elimu Tanzania

Vitabu vingine vya Darasa la Tatu



















ISBN 978-9987-09-950-4



COVER HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI for Sale.indd 1